SUPA JACKPOT
TZS. 1,112,462,859
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Utata** waibuka vifo wanafunzi wakichota maharage kwenye tangi

UKURASA 3

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(COMMERCIAL DIVISION)
AT DAR ES SALAAM

MISCELLANEOUS COMMERCIAL CAUSE NO. 12 OF 2023

IN THE MATTER OF THE COMPANIES ACT 2002 (CAP 212)

AND

IN THE MATTER OF WILEX AUTO TRADING LIMITED
SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION

TO WHOM IT MAY CONCERN

**TAKE NOTICE** that the above petitioner has instituted a suit for winding up petition of the above company, the claim and the particulars of which are set in the petition and service of the summons of the above matter has been ordered by means of publication. You are directed to collect copies of the case documents from the court's Registry, P.O. Box 12533, Dar es salaam.

**ANYONE** concerned is hereby summoned to appear in this court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on **17th May, 2023 at 09:00am before Hon. A.A MBAGWA, Judge** for **orders**. **TAKE FURTHER NOTICE THAT** if should you default to enter appearance as herein provided, the matter will proceed and decision will be given in your absence.

**Given under my hand and Seal of the Court this 5th day of May, 2023.**

DEPUTY REGISTRAR
COMMERCIAL DIVISION
DAR ES SALAAM


# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Mei 14, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581310

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Samia mbogo urasimu vibali minara ya simu

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa , na viongozi wengine, wakishuhudia utiaji saini mikataba ya kupeleka huduma za mawasiliano vijijini kati ya serikali na kampuni za simu za TTCL, Vodacom, Airtel, Halotel na Tigo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA 3

# Kikwete: Membe alikuwa msaada mkubwa kwangu kikazi



Rais mstaafu, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akijadiliana jambo na Bernard Membe, enzi hizo. **PICHA: MAKTABA**



# Simulizi madai mwanafunzi kujiteka kutaka apewe mamilioni

UKURASA. 2

**MICHEZO** YANGA RASMI BINGWA 2022/23 UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia awa mbogo urasimu vibali minara ya simu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa maagizo manane huku akikemea urasimu kwenye utoaji wa vibali vya ujenzi wa minara ya simu na kuagiza kuanzia sasa vitolewe ndani ya mwezi mmoja.

Aidha, ameonya matumizi mabaya ya mitandao kwa vijana na kuwataka watumie kwa kulinda mila, desturi na kujielimisha.

Akizungumza jana kwenye hafla ya kutia saini mikataba ya ujenzi wa minara 758 kati ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na watoa huduma ya mawasiliano nchini, Rais Samia alisema kuna urasimu kwenye utoaji vibali vya ujenzi minara na imekuwa ikichukua miezi sita mchakato wa kibali.

"Sasa tutaitana na wote wanaohusika na mambo haya ya kutoa vibali, vibali hivi vya minara iliyosainiwa leo visizidi zaidi ya mwezi mmoja vibali vyote viwe vimetoka, kuanzia leo hadi Juni 13 nitamuuliza Waziri wamekwama wapi nani amekwamisha."

"Kwa hiyo wale wenye makoti mazito ambayo hayainui mikono kwenye kutoa vibali yainuliwe yawekwe kwenye viti ili mikono iwe myepesi kutoa vibali kisheria kulingana na kanuni tulizojiwekea,"alisema.

Kuhusu tozo zinazolalamikiwa na watoa huduma na kusababisha mabando kuwa ghali, Rais alisema tozo ya kupitisha mkongo kwenye eneo la akiba ya barabara inalalamikiwa ambayo ni Dola za Marekani 1,000.

"Kuna taasisi kadhaa zinatumia maeneo yale tozo zipo chini lakini mkongo ni Dola za Marekani 1,000 kupitisha kwenye maeneo hayo. Sasa hii haiwi bure inakwenda kuingia kwenye gharama za mabando za watu wa simu, ili tushushe gharama na watu wetu wakatumie vizuri huduma kule vijijini lazima serikali tuliangalie hili vizuri,"alisema.

Kuhusu upungufu wa umeme maeneo ya vijijini ambako minara hiyo itajengwa, alisema: "Mnara mmoja kwa mwezi unatumia Sh.Milioni 1.8 tukitumia majenereta lakini tukitumia umeme tunakwenda kutumia Sh.400,000 tu, kwa hiyo tunapaswa kulitazama suala la umeme vijijini."

Aliagiza Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuhakikisha minara hiyo inakuwa na umeme ili kushusha gharama za bando na lisiposhuka watakamatana na watoa huduma.

**FAIDA ZA MINARA**

Rais Samia alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa ahadi ambayo amekuwa akitoa mara kadhaa ya kukuza na kuimarisha sekta ya Tehama kwa vijana na kusukuma maendeleo.

"Kuwapo kwa huduma bora za mawasiliano hususan vijijini ni muhimu sana kiuchumi, kisiasa, kijamii, ulinzi na usalama wa nchi, ujenzi wa minara hii ni kichocheo kikubwa cha mafanikio kutokana na wananchi wote kuguswa na kuwa sehemu ya ukuaji wa uchumi," alisema.

Alisema uwekezaji huo utakuza biashara vijijini na kadhia ya ukosefu wa mtandao inakwenda kuondoka kwa wakulima na wananchi wa maeneo hayo.

"Tunakwenda kubadilisha teknolojia vijijini kwa sasa wakulima wana visimu vya tochi, tukiimarisha mitandao yetu ya mawasiliano wakulima wanakwenda kutoka kwenye tochi wanakwenda kwenye 'touch' (simu janja) kwa sababu zile za touch zitawapa taarifa zote za nchi na za kidunia,"alisema.

Pia, alisema hatua hiyo inakwenda kuimarisha huduma za matibabu mtandao vijijini na kupunguza vifo vya wanawake na watoto wakati wa kujifungua.

Kuhusu huduma za TEHAMA shuleni, Rais Samia aliagiza Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwenye kongamano la sera na mitaala mipya ya elimu kulipeleka suala la TEHAMA ili kupata maoni kwa wananchi.

Naye Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alizitaka kampuni za mawasiliano hapa nchini kuendelea kuwekeza na kuongeza mitaji ya uwekezaji wao ili kuimarisha mawasiliano nchini.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alisema kumekuwapo na malalamiko kuwa mawasiliano ni ghali hasa kwenye simu janja na bando.

Aliomba Serikali kuangalia namna ya kupunguza tozo za kupitisha mkongo wa taifa ambazo ni dola za Marekani 1,000 na kusema gharama hizo zimekuwa zikichangia kuongezeka ghamara kwa wananchi.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya habari, Nape Nnauye, alisema kupitia UCSAF imefikisha mawasiliano kwa watanzania zaidi ya milioni 15 wanaoishi vijijini.

"Hadi sasa UCSAF imeingia makubaliano na kampuni za kufikisha huduma za mawasiliano vijijini kata 1,258 zenye jumla ya vijiji 3,704 na wakazi milioni 15.1, jumla ya minara ya mawasiliano 1,380 itajengwa katika mikataba 19 ambayo mfuko umeingia na watoa huduma za mawasiliano,"alisema.

Alisema serikali imetoa ruzuku ya Sh. Bilioni 199.9 na ni ushahidi wa jinsi serikali inavyothamani na kuhakikisha kuwa watanzania hasa wa vijijini wanapata huduma za mawasiliano.

Nnauye alisema asilimia 93.4 ya miradi iliyotangazwa imechukuliwa na kwamba awali ilikuwa inaishia asilimia 60.

"Tulitangaza zabuni za minara 763 tumepata watoa huduma katika kata 713 sawa na asilimia 93.4, katika kata 50 zilizobaki tutakaa chini na watoa huduma nina hakika watoa huduma watafikiria kuzichukua hizi kata changamoto ni kwamba zina wakazi kidogo nao wanahitaji huduma hii,"alisema.

Waziri huyo alisema serikali kupitia UCSAF imekuwa ikitoa ruzuku ya asilimia 40 na watoa huduma huchangia asilimia 60 iliyobaki ya mradi.

# Mwanafunzi adaiwa kujiteka kutaka mamilioni

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MWANAFUNZI Kenedy Nyangige (20) wa Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afya na Sayansi Shirikishi Bugando (CUHAS), anashikiliwa na polisi mkoani hapa kwa madai ya kujiteka kisha kuushinikiza uongozi wa chuo na makundi mbalimbali kutuma Sh. milioni 3.5.

Watu wengine walioshinikizwa kutuma kiasi hicho cha fedha na mwanafunzi huyo wa mwaka wa kwanza anayesoma kozi ya famasia ni wazazi, jamaa na marafiki kwa madai kwamba asiuawe na waliomteka, hali iliyozua taharuki.

Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu msako wa wahalifu uliokamata watuhumiwa 125 kwa tuhuma mbalimbali.

"Mei 5, mwaka huu, majira ya saa 13:00 mchana tulipokea taarifa kutoka kwa Matiko Sirari (29) ambaye ni daktari wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando kuwa mwanafunzi wa mwaka wa kwanza, Kenedy anayesoma kozi ya famasia chuoni hapo, ametekwa na watu wasiojulikana na haifahamiki yuko wapi,"alisema Mutafungwa.

Alisema taarifa hiyo ilieleza kwamba baada ya watu hao kumteka walianza kutumia simu yake wakitaka watumiwe Sh. milioni 3.5 ili wamwachie na endapo haitatumwa watamwua.

Baada ya taarifa hizo, alisema uchunguzi ulifanyika na polisi walipofika eneo ambalo mnara wa simu unasoma, walibaini kuwa kijana huyo alikuwa anadanganya kwa kuwa hakutekwa na mtu yeyote bali alitaka kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu.

"Polisi walibaini mwanafunzi huyo alikuwa kwenye nyumba ya kulala wageni ya FM Katapila, iliyoko Igogo wilayani Nyamagana mkoani hapa, akiwa amejifungia ndani ya chumba namba 103 huku akiendelea kunywa pombe aina ya Balimi," alisema Mutafungwa.

Kuhusu operesheni za kuwasaka wahalifu, Kamanda Mutafungwa alisema wanamshikilia Juma Shija na wenzake 20 wote wakazi wa wilayani Magu, wakiwa na vitu mbalimbali zikiwamo pikipiki mbili na luninga mbili.

Pia alisema wanamshikilia Ravi Sadma kwa tuhuma za kuzalisha mifuko ya plastiki katoni 39 katika kiwanda cha Vira 2018 Company kilichoko wilayani Ilemela.

Alisema wafanyabiashara tisa akiwamo Joseph Nyaking'ono (39), mkazi wa Kisesa wilayani Magu wanashikiliwa kwa tuhuma za kukutwa na zana haramu za uvuvi aina ya nyavu za Timba tano, zilizokuwa zimehifadhiwa kwenye gari yenye namba za usajili T 930 DEQ aina ya Toyota Harrier.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MOROGORO
MKOA MOROGORO
MAOMBI ARDHI NA. 109 MWAKA 2023
NZIACHARO PAULO NZICHARO & OTHER......MWOMBAJI
ATHUMAN RAMADHAN & OTHERS........MJIBU MAOMBI

**POPOTE ULIPO**

Unatakiwa ufike katika Baraza la Nyumba na Ardhi ilioko Wilaya Morogoro terehe 16/05/2023 Saa 2:00 Asubuhi ambapo shauri lako limepangwa kutajwa.

Endapo hutofika wewe binafsi ama muwakilishi wako shauri taja litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi
Imesainiwa leo tarehe 09/05/2023

MWENYEKITI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI
Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA
Usimamizi wa mirathi Na.28/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU LENJONUS FRANCIS NYOMOLELO WA Chang'ombe
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SALUMU LENJONUS NYOMOLELO

**TANGAZO**
(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 03 Mwezi 05 Mwaka 2023

**KUPOTEA KWA CHETI**



**EINOTH PENDAELI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **NS5203/0014/2016** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **LEKULE GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **WMB/RB/78/2023**

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
Probate and Administration Cause No 47 of 2023
In the matter of the late JULIUS MTEMI CHIMOMBO of Nala within Dodoma City
And
In the matter of application for letters of administration by MARISELINA ERNEST CHIMOMBO
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 day May..........2023
Dated at Dodoma this 10 day May..........2023

RESIDENT MAGISTRATE

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
Probate and Administration Cause No 42 of 2023
In the matter of the late ABEL VUNJAMBAO SWALLE of kikuyu within Dodoma City
And
In the matter of application for letters of administration by ERASTO ABEL SWALLE and LILIAN ABEL SWALLE
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 7 day of 6............... 2023
Dated at Dodoma this 2 day of May........2023

RESIDENT MAGISTRATE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MOROGORO
MKOA MOROGORO
MAOMBI YA ARDHI NA. 109 MWAKA 2022
NZIACHARO PAULO NZIACHARO & OTHER.....MWOMBAJI
ATHUMAN RAMADHANI & OTHERS........MJIBU MAOMBI
WITO/KUITWA SHAURINI
ATHUMANI RAMADHANI AND FABIAN JOHN

**POPOTE ULIPO**

Unatakiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Morogoro terehe 16/05/2023 Saa 2:00 Asubuhi ambapo shauri lako limepangwa kutajwa.

Endapo hutofika wewe binafsi ama muwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi
Imesainiwa leo tarehe 09/05/2023

MWENYEKITI

HABARI KITAIFA

# Daktari 'feki' mbaroni akidaiwa kukutwa na vifaa kutoa mimba

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi mkoani hapa linamshikilia, Mohamed Abdallah (43), mkazi wa Morogoro kwa tuhuma za kutoa huduma ya afya kinyume cha sheria, sambamba na kukutwa na vifaa vya kutolea mimba.

Mtuhumiwa huyo alikamatwa Alhamisi wiki hii katika kijiji cha Mapogolo kata ya Milo, wilayani Ludewa majira ya saa 12:00 jioni.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Butusyo Mwambelo, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, amethibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo huku wakiendelea kukamilisha baadhi ya taratibu ili kufikishwa mahakamani.

Alisema baada ya taarifa za awali, kuliwekwa mtego katika eneo la nyumba anayofanyia shughuli hizo lakini hawakumkamata na kubaini yuko kata ya jirani ya Mlangali.

Kamanda Mwambelo alisema walimkuta mtuhumiwa huyo akiwa baa anakunywa pombe na kurejea naye katika eneo lake la kazi na kuanza kufanya upekuzi.

"Tunamshikilia kwa makosa ya kutoa huduma bila kibali kwa sababu amefungua zahanati bubu na amekutwa na vitu mbalimbali. Kwa hiyo upelelezi ukikamilika atafikishwa mahakamani," alisema.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Dk. Leslie Mhagama, alisema mtuhumiwa alipoulizwa kuhusu taaluma yake, alidai kuwa na elimu ya msalaba mwekundu.

Alisema katika upekuzi uliofanyika, mtuhumiwa huyo alikutwa na vifaa mbalimbali vikiwamo vya kusaidia kutoa mimba na kuunganisha mifupa.

"Tumeona mabomba ya sindano yaliyotumika kwa kuchoma watu ambayo yanafika 100. Kwa hiyo inaonekana amechoma watu wengi. Tumeona chombo kinachotumika kuingiza sehemu za siri kwa mwanamke ili kuangalia kilichomo ndani, kwa hiyo alikuwa anatoa mimba," alisema.



Mjane Magreth Katabazi (katikati), akiwa amewashika watoto wake mapacha, Neema Abel na Rehema Abel wenye umri wa mika 18, waliopooza miguu, mikono na kupata changamoto ya kuongea kwa zaidi ya miaka mitatu sasa kutokana na matatizo ya uti wa mgongo na ubongo, katika Mtaa wa Nyambiti, Kata ya Buzuruga, jijini Mwanza juzi, ambapo ameomba msaada kwa wasamaria wema kugharimia vipimo na matibabu yao yanayogharimu zaidi ya sh. milioni 40 kwa wote wawili. Kwa yeyote atakayeguswa awasiliane na mama yao kwa namba 0745405899. **PICHA: VITUS AUDAX**

## Utata waibuka vifo vya wanafunzi wakichota maharage kwenye tangi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANAFUNZI wawili wa Kidato cha Nne katika Shule ya Sekondari Kisomachi iliyoko Vunjo, Moshi mkoani Kilimanjaro, wamefariki dunia kwa madai ya kukosa hewa baada ya kuingia kwenye tanki la kuhifadhia maharage ili kuyachota kutokana na tundu linalotumika kuziba.

Kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi Mkoa wa Kilimanjaro linawashikilia watu watatu akiwamo Mkuu wa Shule hiyo kwa tuhuma za kusababisha vifo vya wanafunzi hao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Simon Maigwa, alisema jana kuwa wanafunzi hao, Edson Mosha na Godwin John, wote wakiwa na umri wa miaka 17, walifariki dunia juzi majira ya jioni baada ya kuingia ndani ya tangi hilo.

"Tunawashikilia watumishi watatu wa shule hii kwa uchunguzi zaidi kutokana na vifo vya wanafunzi wawili ambao inadaiwa waliingia kwenye tangi kwa nia ya kuchota maharagee baada ya njia ya awali kuziba.

"Tukio hilo limetokea Mei 12 (juzi) majira ya saa 10:00 jioni. Wanafunzi hao waliingia ndani ya tangi linalotumika kuhifadhia maharage kwa lengo la kutoa maharage baada ya sehemu ya chini inayotumika kuyatoa kuziba," alisema.

Kamanda Maigwa alisema baada ya wanafunzi hao kuingia humo walikosa hewa na walitolewa na kupelekwa katika Kituo cha Afya cha Kirua Vunjo na walibainika wameshafariki dunia.

"Miili ya marehemu imehifadhiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mawenzi kwa uchunguzi zaidi wa kitaalam," alisema. Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kileuo, Godfrey Mrema, alisema baada ya kupata taarifa hizo, walifika shuleni hapo na kuona mazingira ya watoto kufariki dunia ambayo yaliwapa utata.

"Tulishangaa kuona watoto wamefikaje kwenye ghala la chakula bila mwalimu wa chakula, wala wa zamu au mpishi. Pia mazingira ya kupanda hadi kuingia kwenye tangi hilo bado hayaelezeki. Sijafahamu familia za watoto hao, ninafuatilia ili kujua zaidi," alisema.

## Wakamatwa madai kufanya ushoga, usagaji

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mwanza linawashikilia wanaume wawili waliojitambulisha kwa majina ya Asmath Abdalah na Sharifa Elkana wakiwa na mavazi ya kike wakijiuza mitaani.

Baada ya kuwahoji walibainika kuwa majina yao halisi ni Ismer Abdalah na Jeremiah Elkana na kwamba watu hao wanadaiwa kujihusisha na biashara ya ngono kinyume cha maumbile katika eneo la hoteli ya Villa Park.

Sambamba na watu hao, jeshi hilo linamshikilia Salome Rashidi (23) kwa tuhuma za kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Imedaiwa kuwa wanaume hao wawili walikamatwa kwa nyakati tofauti kutokana na msako wa polisi katika maeneo mbalimbali mkoani hapa na kukutwa pamoja na baadhi ya wanawake katika hoteli ya Villa Park walikokuwa wakifanya biashara ya kuuza miili yao nje ya hoteli hiyo kinyume cha sheria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kutokana na misako mbalimbali iliyofanywa na jeshi hilo kwa lengo la kudhibiti vitendo vya kihalifu na uvunjifu wa sheria mkoani hapa. Kamanda Mutafungwa alisema baada ya kuwakamata wanaume hao ambao walikutwa katika kundi moja na wanawake ambao wamekuwa wakikamatwa mara kadhaa na baada ya kufikishwa polisi kabla ya kuwekwa katika mahabusu ya wanawake, waliwakagua na kubaini kuwa ni wanaume hivyo kuhojiwa upya na kueleza majina yao halisi.

Aidha, Mutafungwa alisema watuhumiwa hao wanaendelea kuhojiwa na baada ya ushahidi kukamilika watafikishwa mahakamani ili kujibu tuhuma za kuruhusu kuingiliwa kinyume na maumbile sambamba na kufanya biashara ya kuuza miili yao kinyume cha sheria.

Pia alisema Salome Rashidi mkazi wa Kisesa, alikamatwa nyumbani kwake baada ya polisi kupokea taarifa kutoka kwa jirani zake kuwa anajihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Mutafungwa pia alisema jeshi hilo linawashikilia pia wanawake wengine ambao hakuwataja idadi waliokuwa wakifanyiwa mapenzi ya jinsia moja na mwanamke huyo na uchunguzi ukikamilika watafikishwa mahakamani.

# LHRC yatoa mapendekezo uboreshaji rasimu ya elimu

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimetoa mapendekezo 10 kwa lengo la kuboresha Rasimu ya Sera ya Elimu ambayo imetangazwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, alitaja mapendekezo hayo kuwa ni kutaka nafasi za maofisa elimu, utamaduni, taaluma, teknolojia ya habari na mawasilianio (TEHAMA) na maofisa elimu sekondari watambuliwe na sera.

"Taasisi hizo hazitambuliwi na rasimu ya sera, licha ya nafasi kuwapo katika mfumo wa elimu, tunapendekeza zitambuliwe," alisema.

Katika pendekezo la pili, alisema kituo hicho kinataka rasimu ya sera itoe ufafanuzi wa kina juu ya dhana ya elimu isiyo katika mfumo rasmi ni elimu ya namna gani, ili kuondoa mkanganyiko uliopo sasa.

"Rasimu ya sera ieleze ni namna gani wanafunzi waliopitia katika mkondo wa elimu isiyo rasmi watatambuliwa kwenye mfumo wa elimu rasmi, " alisema.

Alitaja pendekezo la nne kuwa rasimu ieleze endapo sera itatumika katika elimu ya juu ili kuondoa mkanganyiko uliopo, katika sera ya elimu ya sasa kutokana na kutoweka bayana kama inatumika katika ngazi ya elimu ya juu au haitumiki.

"Tunaomba rasimu hiyo ifungamanishwe na sera nyingine zinazoongelea kwa namna moja ama nyingine ujuzi na maarifa kama vile sera ya sayansi na teknolojia, sera ya viwanda vidogo vidogo ili kuwa na zao la wahitimu wenye ujuzi na maarifa," alisema.

Pia alisema kituo hicho kinapendekeza muda wa kutosha wa kupitia, kuchambua, kuchakata na kufanya mapitio ya rasimu ya sera utolewe kwa wadau, tofauti na sasa ambapo wizara imetoa wiki tatu.

Alitaja pendekezo la saba kwamba ni kutaka kuwepo kipengele cha kufanya tathmini kila baada ya miaka 10 kuhusu utelekelezaji wa sera, huku pendekezo la nane likiwa ni kutaka dhana ya elimu bure kuwekwa wazi.

"Ukweli ni kwamba lugha inayotumika katika rasimu, inaashiria dhana ya elimu bila malipo kutokuwa bure kiuhalisia, lugha inayotumika inaashiria dhahiri shahiri kuwa elimu hiatakuwa bure, bali kutakuwa na michango kadhaa," alisema.

Katika pendekezo la tisa, alisema LHRC inataka rasimu hiyo itoe mwongozo wa adhabu ya viboko, kwa madai kwamba haijagusia suala hilo.

Mkurugenzi Mtendaji huyo alitaja pendekezo la 10 kuwa ni suala la wanafunzi wa kike kurudi shuleni baada ya kupata ujauzito, kwamba liwe la kisera, Kwa kuwa rasimu hiyo haijalizungumzia.

"Kimsingi, rasimu hii na mambo mazuri, hivyo tushirikiane kuhakikisha Inaboreshwa kwenye baadhi ya maeneo ambayo tumeyataja, ili kuboresha elimu yetu," alisema.

Aidha, alisema LHRC inakubaliana na pendekezo la rasimu ya sera ya elimu kuhusu ukomo wa elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu.

" Rasimu ya Sera ya Elimu toleo la mwaka 2023, linapendekeza kuwa na mfumo wa elimu wa 1+6+4+2/3+3+, kwa maana ya kwamba elimu ya awali itakuwa kipindi cha mwaka mmoja," alisema.

Alifafanua kuwa elimu ya msingi itakuwa kwa kipindi cha miaka sita, sekondari itabaki kuwa ya miaka 4 kidato cha kwanza hadi cha nne, huku kidato cha tano na sita ikiwa ni miaka miwili.



Diwani wa Kata ya Kisukuru, Lucy Lugome (wa pili kulia), akipokea risala kutoka kwa Mwanachama wa kikundi cha vuguvugu la kumkomboa mwanamke kifikra kiitwacho Mapambano TAPO, Nduna Mani katika hafla ya uzinduzi wa kikundi hicho, jijini Dar es Salaam jana. Wa (tatu kulia) ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kisukuru, John Msele. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA.**

# Kikwete: Membe alikuwa msaada mkubwa kwangu kikazi na kisiasa

**Na Romana Mallya**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, amefunguka kuhusu aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Bernard Membe, kwamba alikuwa mtu wa msaada mkubwa kwake katika maisha ya kikazi na kisiasa.

Kikwete amesema wametoka mbali na Membe, alitumika katika wadhifa huo kwa miaka minane wakati wa serikali yake, wamesaidiana kwa mengi.

Membe alifariki dunia juzi asubuhi katika Hospitali ya Hurbert Kairuki, Mikocheni mkoani Dar es Salaam alipokuwa akipatiwa matibabu baada ya kuzidiwa ghafla.

Viongozi mbalimbali wa serikali, taasisi, vyama vya siasa jana waliendelea kumiminika nyumbani kwa marehemu Membe Mikocheni kwa ajili ya kuhani msiba huo.

Katika salamu zake za rambirambi alizozitoa juzi kwa mke wa Membe, Mama Dorcas Membe, Kikwete amefunguka mambo mbalimbali.

Katika taarifa yake, Kikwete alisema, "Familia zetu na mapito ya maisha yetu yamehusiana sana."

Alisema Membe alikuwa mtu wa msaada mkubwa kwake katika maisha yake ya kikazi na kisiasa.

"Nilimwamini na kumtumainia katika nafasi zote alizohudumu kwenye baraza langu la mawaziri.

"Aliwahi kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Nishati na Madini. Hali kadhalika, aliwahi kuwa Waziri wangu wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa miaka tisa ambapo alifanya kazi kubwa na nzuri ya kuendeleza maslahi ya Tanzania katika medali za kimataifa," aliandika Kikwete na kuongeza:

"Ninautambua mchango wake mkubwa aliotoa kwenye Chama Cha Mapinduzi alipokuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Mjumbe wa Kamati kuu na Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa katika Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa. Katika nafasi zote hizo, alijitoa kwa moyo wake wote na kuacha alama za kudumu," alisema.

Pia alisema anamfahamu Membe kama mwanadiplomasia mbobezi, mwanamikakati makini, msomi mzuri, mcha Mungu, mzalendo, mchapakazi hodari na mtu jasiri ambaye hakuogopa kusema na kulisimamia analoliamini.

"Hakika taifa limepoteza mmoja wa watu muhimu. Ninatoa salaam za rambirambi na mkono wa pole kwako shemeji yangu, Dorcas Membe na watoto wetu, Cecilia, Richard na Dennis pamoja na wajukuu, ndugu na jamaa wa marehemu Membe. Nawapeni pole kwa msiba mkubwa uliowakuta.

"Lakini, ninapenda kuwahakikishia kuwa hamko wapweke. Mimi pamoja na mke wangu Salma na wana familia wetu wote, tuko pamoja nanyi katika majonzi na kuomboleza. Tunawaombea kwa Mola awajalie moyo wa subira na ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu mnachopitia," alisema. Kikwete akamalizia kwa kusema: "Tukumbuke daima sisi sote ni waja wake, na kwake tutarejea'. Bwana ametoa Bwana ametwaa, Jina lake lihimidiwe. Tumwombee kwa Mola marehemu mpendwa wetu, apumzike kwa amani na roho yake aiweke mahala pema peponi. Amina."

Katika Wizara Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (sasa Wizara ya mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki), Membe alihudumu kama Waziri kwa miaka tisa hadi 2015, akiwa mtu wa pili kushika wadhifa huo kwa miaka mingi, akitanguliwa na Kikwete aliyeshika kwa miaka 10.

**MPANGO ATOA POLE**

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kupitia ukurasa wake wa Instagram aliandika: "Ninaungana na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, kutoa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na watanzania kwa ujumla kufuatia kifo cha aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje, marehemu Bernard Membe.

"Mwenyezi Mungu akawe mfariji wa familia na wote walioguswa na msiba huu. Ninamuombea marehemu apumzike kwa amani."

Akizungumza nyumbani kwa marehemu, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, alisema tofauti zao za kiitikadi hazikuutofautisha ukaribu wake na kwamba yalikuwapo mambo waliyoshirikiana.

Alisema licha ya kero alizowahi kufanyiwa na serikali ya CCM haiondoi ukweli kuwa bado wana uhusiano na baadhi ya viongozi wake.

Kiongozi huyo wa CHADEMA alisema Membe alikuwa mtu asiyekasirika na hata ikitokea hivyo alionyesha tabasamu.

HABARI KITAIFA

# Mwigulu ataka utafiti vikwazo vigezo mtangamano wa uchumi

**Na Benny Mwaipaja,** ARUSHA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amezishauri nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kufanya utafiti ili kufahamu sababu za nchi hizo kushindwa kufikia vigezo mtangamano wa uchumi mpana.

Vigezo hivyo ni sehemu ya nchi hizo kufanikisha itifaki ya Umoja wa Sarafu wa EAC ifikapo mwaka 2031. Dk. Nchemba alitoa rai hiyo juzi wakati wa mkutano wa 15 wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Fedha na Uchumi la EAC uliofanyika jijini hapa.

Pamoja na mambo mengine, mkutano huo ulipokea na kujadili taarifa mbalimbali za mkutano uliopita wa baraza hilo.

Miongoni mwa ajenda zilizojadiliwa ni pamoja na mashauriano ya kibajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24, taarifa ya Mkutano wa 26 wa Kamati ya Magavana wa Benki Kuu za Jumuiya hiyo; mwenendo wa hali ya uchumi na maendeleo duniani pamoja na hatua zilizofikiwa na nchi wanachama katika kukidhi vigezo vya mtangamano wa uchumi mpana wa jumuiya.

Alisema Tanzania imekidhi vigezo vyote vya mtangamano wa uchumi mpana isipokuwa kigezo cha nakisi ya bajeti kinachopaswa kuwa chini ya asilimia tatu. Kwa Tanzania kigezo hicho kimefikiwa kwa asilimia 3.3 wakati nchi zote za jumuiya hiyo zimeshindwa pia kufikia kiwango kinachotakiwa ili kuwezesha kufikiwa kwa umoja wa fedha unaolenga kuwa na sarafu moja.

"Tathmini inaonyesha kuwa nchi wanachama hazikufikia vigezo vyote vya msingi vya mtangamano wa kiuchumi kutokana na changamoto mbalimbali zikiwamo UVIKO-19 na ongezeko la mahitaji ya rasilimali fedha kwa nchi wanachama katika kuendelea kuwekeza kwenye miundombinu muhimu kwa jamii," alisema.

Dk. Nchemba alishauri Baraza la Mawaziri wa Fedha na Uchumi kuielekeza Sekretarieti ya EAC kufanya utafiti kuhusu kukwama kwa nchi zote wanachama kufikia kigezo hicho na kuchambua na kuandaa mwongozo wa sera utakaoziwezesha kutatua kikwazo hicho. Suala la nchi wanachama kufikia vigezo vya mtangamano wa uchumi mpana ni muhimu katika kufanikisha itifaki ya Umoja wa Sarafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Baadhi ya nchi wanachama zimekuwa hazifikii malengo katika kufikia vigezo hivi na kumekuwa hakuna hatua zinazochukuliwa ili kuhakikisha nchi zote wanachama zinafikia vigezo kabla ya kuwa na sarafu moja ifikapo 2031," alisema.

Mapendekezo ya Dk. Nchemba yaliungwa mkono na Mawaziri wa Fedha na Uchumi wa Kenya, Rwanda, na Burundi na wawakilishi wa mawaziri wa fedha wa Sudan Kusini na Uganda. Walisema kutokana na vigezo hivyo kuwekwa muda mrefu na kushindwa kufikiwa kunamaanisha kuna haja ya kuviangalia upya.

## Ongezeko mashtaka ukiukaji madili latisha

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, amesema kumekuwa na ongezeko la mashtaka yanayogusa maadili nchini huku asilimia 40 yaliyopokewa hadi juzi katika Mahakama ya Wilaya ya Kigamboni ni ya mmomonyoko wa maadili.

Mwakitalu alibainisha hayo juzi jijini hapa kwenye kikao kazi cha kukusanya maoni ya mapitio ya sheria zinazosimamia makosa dhidi ya maadili Tanzania kilichowakutanisha wakuu wa upelelezi wa jinai Tanzania Bara na Zanzibar na waendesha mashtaka wa mikoa yote nchini kilichoandaliwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania.

Alisema ni muhimu kujadili kwa kina kwa kuwa tatizo ni kubwa.

"Kikao hiki ni muhimu sana kwa sababu kitatoa mwanga na kuonyesha njia ya kupata ufumbuzi wa namna bora ya kukabiliana na majanga ya namna hii ambayo yanalikabili taifa,"alisema.

Mwakitalu aliwaomba washiriki wajadili kwa wazi na kina, kwa sababu maazimio ya kikao kazi hicho yatakuwa na matokeo chanya kwenye kupata sheria bora zinazosimamia maadili nchini.

Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Naibu Kamishna (DCP) Salehe Ambika, alisema waendesha mashtaka na wakuu wa upelelezi wanapaswa kutoa maoni na mapendekezo ili kama sheria zilizopo zina upungufu zirekebishwe.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Griffin Mwakapeje, alisema kwa sasa wameanza utafiti na mapitio ya sheria zote zinazosimamia makosa dhidi ya maadili.

"Makosa haya ni yale yanayohusisha kubaka, genge la ubakaji, kujaribu kubaka, kuteka, udhalilishaji wa kingono, kuwaingilia kingono watu wenye ugonjwa wa afya ya akili, kumuingilia mtu asiye mke mwenye umri chini ya miaka 18 bila ridhaa yake, kuwatweza watoto kingono,"alisema.

Alitaja mengine kuwa ni udhalilishaji mkubwa wa kingono, uwakala wa ukahaba, kumiliki madanguro, kuingilia kinyume na maumbile (ushoga), kuzini na maharimu, kusambaza picha za ngono, ponografia kwa watoto na kwa njia ya mtandao, usagaji na mengine yanayofanana na hayo.



Mbunge wa Jimbo la Kawe na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Askofu Dk. Josephat Gwajima (wa pili kushoto), akikagua zoezi la ugawaji wa vifaa mbalimbali vya kuunganisha maji linaloendeshwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) kwa wananchi wa eneo la Mivumoni, Kata ya Wazo, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana. Mbunge huyo, yupo katika ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo jimboni kwake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## Mikopo umiza kichocheo uvunjifu wa ndoa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya wanawake mkoani Shinyanga ambao wamekuwa wakishiriki katika mikopo kutoka katika taasisi mbalimbali maarufu kama 'Mikopo Umiza' au 'Kausha Damu' wamesema imekuwa ikisababisha ndoa zao kuvunjika hususani wakati wa urejeshaji.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wanawake hao walisema tatizo kubwa limekuwa riba kubwa inayohitajika ilhali mitaji yao ni midogo kumudu urejeshaji wa mikopo hiyo.

Zai Abdul, mkazi wa Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga, alisema wamekuwa wakikopa fedha huku wakiwa hawana biashara hali ambayo imekuwa ikisababisha fedha inayokopwa kutumika kufanyia matanuzi binafsi na ukifika wakati wa marejesho hali inabadilika na kusababisha migogoro ya kifamilia.

Kulwa Juma, mkazi wa Kambarage, Manispaa ya Shinyanga, alisema yeye nusura avunje mji wake baada ya mke wake kwenda kukopa bila kumshirikisha huku akiwa hana hata biashara yoyote.

"Siku moja nilishangaa kuona watu wanaingia ndani na kuchukua kila kitu kwa kile kinachodaiwa kuwa ni mkopo aliochukua mke wangu. Ilinibidi nitulize akili na kuacha kuchukua uamuzi wa haraka tofauti na hivyo, ndoa ingevunjika," alisema Juma.

Tatizo kubwa katika mikopo hiyo ni kutokana na wanawake kukopa bila kuwashirikisha waume zao lakini wanapokwama kurejesha, wakopeshaji huamua kufilisi kaya husika bila kujali kama familia zima inaelewa. Hapo ndipo migogoro ya familia inapoanza kutokea na kufikia hata ndoa zingine kuvunjika.

Akithibitisha kupokea kesi mbalimbali juu ya tatizo hilo, Mwenyekiti wa Mtaa wa Dome, Kata ya Ndembezi, Solomon Najulwa, alisema migogoro mingi imekuwa ikisababishwa na baadhi yao kutokuwa wakweli na kutoa taarifa za uongo kuwa hawajaolewa, huku wao wakiwaandikia barua na kuwagongea mihuri ya udhamini.

Aidha, alisema wengine huandika maelezo ya uongo ili kuja kuumbuka wanapokwama kurejesha mikopo hiyo. Muda mwingine wanatumia mkopo huo kulipa mkopo mwingine na kuwafanya washindwe kuwa na maendeleo.

"Unakuta mwanamke ana mikopo zaidi ya mitano na biashara hana na dhamana ambayo ameweka kwenye mikopo hiyo ni vitu vile vile ambavyo aliweka katika mkopo wa kwanza. Akibanwa marejesho anakwenda kukopa kwingine ili apunguze deni, hivyo anajikuta ana madeni lukuki," alisema Najulwa.

Kuhusu takwa la kisheria kwa masuala hayo wakati akizungumza na Nipashe, Teresia Fabiani, mwanasheria kutoka LEAT, alisema Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 na Sheria ya Kuweka Mali Rehani ya mwaka 2008, zinasema mwanamke au mwanamume akienda kukopa bila makubaliano ya mke au mume, mkopo huo ni batili na hata mali haipaswi kuchukuliwa kwa sababu mkataba hauna makubaliano ya pande mbili.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utoaji Mikopo ya Msilikale, Robert Prosper, alitaja taratibu za ukopeshaji kwamba wanawake huwa wanafika na wadhamini wao pamoja na barua kutoka kwenye uongozi wa serikali za mitaa huku wengine wakisema hawajaolewa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wauguzi warejee maadili katika utendaji kazi wao

**WIKI** hii kulikuwa na maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani ambayo kwa Tanzania yalifanyika katika maeneo mbalimbali na kwa staili anuai ikiwamo kutoa zawadi kwa makundi mbalimbali na kupanda miti ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali katika utunzanji wa mazingira.

Maadhimisho hayo ambayo yamekuwa yakifanyika kila mwaka duniani kote, licha ya kumuenzi muuguzi wa kwanza, Florence Nightingale, kutokana na matendo mazuri aliyoyafanya na kuiheshimisha taaluma hiyo, yamekuwa yakitumika kama jukwaa la kukumbushana wajibu wao pamoja na maadili yanayoongoza fani na tasnia kwa ujumla.

Katika maadhimisho ya mwaka huu, mkoani Shinyanga kwa mfano, wauguzi walikumbushwa kufanya kazi zao kwa weledi ikiwamo kuzingatia maadili na kutumia lugha zenye staha kwa wagonjwa badala ya kuwatolea lugha chafu.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Elisha Robert, alisema katika maadhimisho hayo yaliyofanyika kimkoa kwenye Kituo cha Afya cha Kambarage, Manispaa ya Shinyanga kuwa wauguzi wanapaswa kuzingatia maadili na miiko ikiwa ni sehemu ya kumuenzi Nightingale ambaye alikuwa akihudumia wagonjwa kwa upendo, hivyo ni vyema wakafanya hivyo kwa vitendo kutoa huduma bora na kutumia lugha nzuri ambazo pia zinaongeza faraja kwa wagonjwa.

Kiongozi huyo aliwasisitiza kuwa wauguzi wanapaswa kufanya kazi kwa  kumtanguliza Mungu na kuwapokea na kuwahudumia vizuri wagonjwa pamoja na kutumia lugha nzuri, kufanya kazi kwa bidii, ushirikiano na kutumia nafasi zao kupunguza vifo vikiwamo vya uzazi.

Kutokana na rai hiyo, Muuguzi Mkuu wa Manispaa ya Shinyanga, Loyce Nicolao, kwa niaba ya wauguzi wenzake, aliahidi kuwa katika kumuenzi Nightingale, watawahudumia wagonjwa kwa moyo wote, kwa upendo na kujituma, ili kuhakikisha wanapata huduma bora za matibabu na kuokoa afya zao.

Ujumbe huo kwa wauguzi ulikuwa mzito na umetolewa kwa wakati wake kutokana na mazingira ya sasa katika taaluma mbalimbali ikiwamo ya uuguzi. Kwa muda mrefu, wauguzi wamekuwa wakilalamikiwa na wagonjwa kwamba baadhi yao wamekuwa wakidaiwa kushiriki vitendo vya rushwa na kutoa lugha chafu kwa wagonjwa na ndugu zao.

Iko mifano hai ambayo kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia, baadhi ya wauguzi wamekuwa wakirekodiwa katika video fupi na kuonyeshwa kwenye mitandao ya kijamii juu ya mambo wanayoyafanya ambayo kwa kiasi kikubwa yanakiuka miiko na maadili ya kazi zao.

Uko mfano mmoja ambao uliwahi kutoka katika hospitali moja Dar es Salaam. Wauguzi wawili waliokuwa zamu katika wodi husika, walifuatwa na ndugu wa mgonjwa aliyekuwa akiomba msaada. Baada ya kuambiwa, walijibu kwamba wamesikia na watamhudumia lakini wakati ndugu wa mgonjwa alipoondoka, akiwa mita chache kutoka eneo la wauguzi, mmoja alisikika akisema: “Mzee mwenyewe ana miaka 74 wanahangaika naye wa nini?”


Pia wako baadhi ambao wamerekodiwa wakionekana wanaomba rushwa na wengine wakitoa lugha chafu kwa wagonjwa. Wengine pia wamekuwa wakiwaacha wagonjwa wakitaabika vitandani wakikosa msaada kutoka kwa wauguzi huku wakipiga soga, kuchati kwenye simu na hata kutoka kwenye maeneo yao ya kazi na kwenda kuzurura au kufanya mambo binafsi.

Ni vyema wauguzi wakarejea katika majukumu yao kwa kufanya kazi kwa moyo wa upendo kwa sababu wakati mwingine wagonjwa wanapata faraja na hata kupungukiwa na maumivu yanayowasibu kutokana na upendo na faraja kutoka kwa watu wanaowahudumia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hoja ya Prof. Muhongo kuhusu uvuvi wa vizimba ina mashiko

Na Sabato Kasika

**UFUGAJI** wa samaki kwa vizimba, unatajwa kuwa ni njia rahisi na yenye tija kwa wafugaji wa samaki kibiashara na ndio njia ambayo wavuvi wamekuwa wakishauriwa kuitumia ili kupata tija.

Kizimba ni mfumo wa kufugia samaki waliowekwa katika vyavu za kufugia zilizozungushwa kwenye fremu na kutumbukizwa katika kina kirefu cha maji ya bwawa, ziwa au bahari.

Njia hiyo inatajwa kuwa inasaidia kuweka samaki wengi kwenye eneo dogo, na kwamba inafaa zaidi kufuga kibiashara na inahitaji uchaguzi sahihi wa eneo, kwa ajili ya kupata manufaa.

Vilevile yapo mambo ya kuzingatia kabla ya ufugaji huo, ikiwamo kuwa na vibali vya uendashaji wa shughuli za ukuzaji viumbe hai majini, muhtasari wa kikao cha serikali ya kijiji sehemu ambayo mradi utafanyika.

Mengine ni utafiti katika eneo litakalowekwa vizimba, kupima kina cha maji, ubora wa maji, mkondo wa maji, ukubwa wa mawimbi na kupata kibali kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Idara ya Ukuzaji Viumbe Hai Majini. Baadhi ya mambo ya kuzingatia katika uvuvi huo ni vibali vya uendashaji wa shuguli za ukuzaji viumbe hai majini, muhtasari wa kikao cha serikali ya kijiji au mtaa ambapo mradi utafanyika.

Mengine ni utafiti katika eneo litakalowekwa vizimba, kupima kina cha maji, ubora wa maji, mkondo wa maji, ukubwa wa mawimbi na kupata kibali kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Idara ya Ukuzaji viumbe hai majini.

Hayo na mengine yakikamilika, mhusika atatengeneza kizimba na kupanda vifaranga, na kwamba chenye urefu wa mita sita, upana mita sita na kina cha mita sita, kinaweza kubeba vifaranga 10,000 aina ya sato.

Ndivyo Mwongozo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu ufugaji wa samaki kwenye vizimba unaeleza na pia wapo wadau wamekuwa wakiupigia chapuo uvuvi wa njia hiyo kwa manufaa ya wavuvi na taifa.

Miongoni mwa wadau hao ni mbunge wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Profesa Sospeter Muhongo ambaye hivi karibuni aliishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwekeza katika uvuvi wa kutumia vizimba.

Alikuwa akichangia katika hotuba ya bajeti ya Wizaraa ya Mifugo ya mwaka 2023/2024, bungeni jijini Dodoma na kufafanua kuwa sekta hiyo itakuwa na mchango mkubwa iwapo uvuvi kwa njia hiyo utapewa nafasi.

Huku akipigiwa makofi na wabunge wenzake kama ishara ya kukubaliana na hoja yake, alisema uvuvi huo unaweza kusaidia taifa kutoka asilimia nane hadi kufikia asilimia 10.

Kwa mujibu wa Prof. Muhongo, hatua hiyo pia inaweza kusaidia kupunguza umaskini na kwamba hilo linawezekana, kwa kuwa Tanzania ina maziwa makuu matatu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Akifafanua kuwa, maziwa hayo yana samaki wengi wenye soko duniani, akitolea mfano ziwa Tanganyika kuwa lina aina zaidi ya 350 ya samaki, ziwa Victoria aina zaidi ya 500 ya samaki na Nyasa kati ya 800 na 1,000.

Anabainisha kuwa nchi hii ina fursa ya kuwekeza katika uvuvi wa kibiashara kwa kutumia vizimba kwenye maziwa hayo, na kwamba hatua hiyo itasaidia sekta hiyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi.

Uvuvi kwa njia hiyo, umekuwa pia ukionyeshwa katika maonyesho ya Nanenane, hivyo, si vibaya ushauri wa mbunge huyo ukafanyiwa kazi ili wavuvi wanufaike na taifa nalo linufaike.

Mbunge huyo anasema sekta ya uvuvi inaweza kusaidia kukuza uchumi wa nchi kutokana na umuhimu wake. Kwa kuwa njia ya vizimba inaonekana kuwa na tija, basi wavuvi wahamasishwe.

## FIKRA MBADALA

# Buriani mwanadiplomasia nguli Benard Membe



Pascal Mayalla

LEO katika viwanja vya Karimjee, Watanzania tunamuaga aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na mwanadiplomasia nguli, Bernard Membe, aliyefariki dunia ghafla juzi katika Hospitali ya Kairuki, Mikocheni, Dar es Salaam.

Fani yetu ya uandishi wa habari, inatukutanisha na watu mbalimbali, hivyo japo sikumbuki nilikutana vipi kwa mara ya kwanza na Membe, nilipata nafasi ya kuzungumza naye kwa nafasi, wakati wa safari za Mikutano ya Baraza Kuu la Umoja wa mataifa (UNGA) enzi za serikali ya awamu ya tatu chini ya Benjamin Mkapa. Wakati huo nilikuwa mwandishi wa kwanza wa vyombo vya habari binafsi kusafiri na ujumbe wa Tanzania kwenda kuripoti mikutano hiyo New York.

Hapo nilikutana na Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete kwa nafasi. Hata baada ya Kikwete kuingia Ikulu, niliendelea kuripoti UNGA na kukutana na Membe akiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Katika mfululizo wa safari hizo ndipo nikamwona Membe akiwa anazungumza kwa kujiamini sana kwa mamlaka kama ndiye Rais mtarajiwa.

Kuna wakati kupitia kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na ITV, alitutishia sisi waandishi wa habari kwa kutuambia tuombe asioteshwe kugombea urais mwaka 2015. Alisema ikitokea akaoteshwa, kuna maadui zake 11 itawabidi watafute pa kuhamia. Aliwataja miongoni mwa maadui zake hao wakiwamo waandishi wa Habari wawili.

Kwa vile na mimi ni mwandishi wa Habari na niliwahi kuwa 'critical' kuhusu Membe, nilipouliza anawezaje kujua kilichomo ndani ya 'diplomatic bag' ya nchi nyingine, hivyo kuelekea mwaka 2015 ili nisiwemo kwenye list ya kuihama nchi, nikajitolea kumsaidia Membe.

MTU WA WATU

Kuna siku kwenye sherehe fulani ya kumuaga mdogo wake (send off), mwandishi mwenzetu Usia Mkoma, nilikutana na Membe. Ulipofika wakati wa chakula, Membe akienda kwenye bufee (sehemu kilipopangwa chakula) , nilimsalimia kumwambia "tunakuombea Uoteshwe!"

Kwa wanaokumbuka kile kipindi cha Dakika 45 cha ITV, Membe alitoa ole kuwa tuombee asioteshwe, kugombea urais 2015, maana akioteshwa kuna watu watahama nchi.

Baada ya kumtania tunakuombea uoteshwe, akacheka tu, nikamuuliza inakuwaje mpaka leo hajaoteshwa? Akajibu kilichomchelewesha kuoteshwa ni kwa sababu "silali usingizi". Nafanya kazi usiku na mchana, hivyo sipati kabisa muda wa kulala usingizi hadi kuota, ila siku nikipata muda wa kulala usingizi wa kuota ndoto, labda nitaota.

Ni kipindi cha Membe Tanzania ilibadili diplomasia kutoka vita baridi kuwa diplomasia ya kiuchumi. Nilipokutana na Membe, nikamtania kwamba tunafuata vipi diplomasia ya kiuchumi wakati kwenye balozi zetu, bado tunajaza waambata wa kijeshi na wale jamaa zetu wa 'kazi mbili mbili' badala ya kupeleka waambata wa kiuchumi?!. Membe alicheka tu.

Mwaka 2015 nikijua ni Membe, nikamwandalia 'video documentary' nzuri kumfagilia njia ya 2015 na baada ya kuikamilisha nikawapelekea wadau muhimu wa kutoa mpunga wa maana kuidhamini irushwe ili Membe apae. Wadhamini waligoma ndipo nikaanza kuusoma mchezo wa 2015 kuwa kumbe si Membe!

Hivyo kuelekea mwaka 2020, Membe akaamua kutingisha kibiriti. Kuna mwandishi mmoja wa habari akaamua kumchafua, Membe akaibuka na niguse ninuke na kweli akakinukisha na kufukuzwa CCM. Niliandika kitu kumhusu Membe nikamshauri japo ameonewa lakini asifanye uamuzi wa hasira.

Nilimpa ushauri kuwa asihame Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa hasira lakini haikusaidia. Alihama na kujiunga na ACT Wazalendo na kuwa mgombea urais. Baada ya uchaguzi, alijirudi na kurejea nyumbani na akapokewa, akamfungulia kesi yule mwandishi akashinda na mwandishi anatakiwa kumlipa Membe mabilioni ambayo hana.

Mwandishi yule akawatumia baadhi ya maaskofu kumwombea msamaha kwa Membe. Membe akawagomea, sisi watu wa ushauri wa bure pia tukashauri. Huu ni wito wangu na ushauri wangu wa bure kwa Bernard Membe, asibishane na maaskofu, amsamehe tu huyu mwanafani mwenzetu kwa kuwa wakati alipokuwa akiyatenda hayo na kufanya makosa yale.

Tulisema hakuwa yeye bali alikuwa kama amemilikiwa na shetani na akawa anamtumia apendavyo, hivyo baada ya kuombewa, mapepo yamemtoka, ametambua makosa yake, ametubu, ameomba msamaha na kama mwanadamu anastahili msamaha. Hatimaye kabla ya kulipwa mabilioni yake, ndio sasa Membe ameitwa mbele ya haki, na leo ndio tunamuaga.

Kitu cha kwanza ninachosema, kuna uwezekano Membe ndani ya moyo wake alishasamehe, hivyo kama alisamehe, wadeni wake wako salama lakini kama hajasamehe amekufa na kinyongo, namshauri yule mwandishi habari mwenzetu, kwa muda wake, aende kwenye kaburi la Membe na kumwomba msamaha hata kifoni ili amsamehe. Asipofanya hivyo, Membe atafidiwa kupitia kitu kinachoitwa fidia za karma. Kiukweli gharama zake huwa ni kubwa kuliko kitu chochote.

Benard Camilus Membe, umepigana vita vilivyo vitakatifu, Mwendo umeumaliza.

Imani umeilinda. Sisi tulikupenda, lakini Bwana akakupenda zaidi. Bwana alitoa, Bwana ametwaa, Jina lake Lihimidiwe.

**Paskali**
**0754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tumshukuru hivi Rais Samia kwa anayotufanyia



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

MIAKA takriban 10 na ushei hivi, Watanzania walipita kwenye barabara iliyoziba kwa nyasi na mbigiri kwa wingi na kusababisha waliojaribu kupita kwa miguu iliyo wazi kuchomwa na kujeruhiwa.

Barabara hii ilijaribu kuchongwa enzi za Rais Jakaya Kikwete na kupitika, ilijifunga ghafla wakati huo huo wa Kikwete na kusababisha taharuki, huku watu wakidhani akiingia Rais mwingine itafunguka.

Alipoingia Dk. John Magufuli, hakutaka kuichonga kabisa na mbaya zaidi kuamua kumwaga chupa zilizovunjika, hivyo kuzuia kabisa watu kupita, husussan wasio na viatu au wenye viatu dhaifu.

Watu wakasahau kabisa kupita njia hiyo iliyotarajiwa kuwarahisishia safari ya kwenda kununua mahitaji yao kwa haraka lakini wakakata tamaa na kutumia njia zingine za mzunguko.

Alipofariki dunia Rais Magufuli na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani, ghafla majani katika barabara hiyo yakaanza kunyauka na mbigiri kukauka.

Kilichobaki kikionekana ni vipande vya chupa ambavyo vilikuwa dhahiri wazi. Lakini juzi Rais Samia aliviona na sasa kutaka viondolewe na barabara hiyo isafishwe ili watu waitumie kufuata mahitaji yao kwa haraka na amani.

Barabara hiyo inaitwa Mt. Katiba Mpya. Juzi akaitisha kikao maalumu cha Baraza la Vyama vya Siasa kupitia kwa Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi.

Kikao hicho ni cha kutathmini utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi Kazi kilichoratibu maoni ya watu kuhusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini, kuelekea mchakato wa kusafisha barabara yetu hiyo.

Mbali na mchakato huo, mambo mengine muhimu yatakayojadiliwa ni mabadiliko ya sheria mbalimbali kuhusu uchaguzi; zikiwamo sheria za Tume ya Taifa ya Uchaguzi na ya vyama vya siasa.

Hii ni dhahiri kuwa Rais Samia ana nia na dhamira njema kwa Tanzania na watu wake. Inamaanisha Rais Samia hana tamaa ya kuwa na mkono wa chuma kwamba yeye kwa kuwa Rais basi ndiye kila kitu.

Anaonekana hataki kusikia kauli za 'atake asitake' au 'aongoze milele' na zingine kama hizo, zilizohanikizwa na 'chawa' wasiojiamini, wakitaka kujikomba kwa uongozi wa juu huku wananchi wakiumia.

Nani asiyeuona mwelekeo wa taifa hili chini ya Rais huyu aliye katika umbile la mwanamke ambaye kwa muda mfupi tu madarakani, amezidi baadhi ya viongozi wa maumbile ya kiume.

Hiyo ni kutokana na hekima na busara zinazomtawala katika uongozi wake, akifikiria kabla ya kutenda, huku pia akiona Watanzania kama ndugu na watu wake wa karibu bila kujali tofauti za kiitikadi, rangi, kabila na dini.

Haya anayoyafanya Rais Samia yanayoendana na matakwa na matamanio ya Watanzania wengi, yanamfanya aonekane kama mtu aliye tayari hata kutafutiwa nyumba Tabata, ili aishi na Watanzania wenzake bila wasiwasi.

Anaonekana kuongea lugha moja na Watanzania walio wengi katika masuala ya haki, amani, utulivu, umoja na mshikamano. Vinginevyo, asingekaa meza moja na kina Freeman Mbowe wala asingehudhuria mkutano wa BAWACHA!

Lililobaki sasa kwa Watanzania ni kuendelea kutoa ushirikiano wa dhati kwa Rais wao huyu rahim, na kuhakikisha wanapita salama katika barabara hiyo aliyoamua kuisafisha na kuichonga vizuri hata kuitamani.

Kwa hatua hii, kwa maoni yangu, naamini tutapoteza rasilimali fedha iwapo tutaendesha uchaguzi wa kumpata Rais mwingine mwaka 2025; kwani inatosha kumruhusu aendelee mpaka 2030 nje ya sanduku.

Namaanisha uchaguzi wa 2025 uhusu wabunge na madiwani peke yao ili tumpe wabunge wazuri kutoka itikadi zote, naye awe na fursa pana ya kupata mawaziri watakaomfaa, kuliko wengi alionao sasa ambao kwa njia moja au nyingine wanamtwisha mizigo mizito.

Si siri kwamba kwa mujibu wa Katiba, analazimika kupata mawaziri kutokana na wabunge walioingia bungeni mwaka 2020 katikati ya lindi la malalamiko na manung'uniko ya wapiga kura na hata baadhi yao kukataa kuutambua kuwa halali.

Ni dhahiri kama tuliweza kufuta sherehe mbalimbali ikiwamo kubwa ya Uhuru wetu uliotufungua minyororo ya Ukoloni, tutashindwa nini kufuta uchaguzi wa urais na kubakiwa na wa wabunge na madiwani, kama njia ya kumshukuru Rais Samia kwa haya anayotufanyia. Ruksa kupinga hoja hii lakini kwa hoja.

**Alamsiki!**

## Tigo Mastercard yarahisisha mambo

**Na Mary Geofrey**

HUDUMA ya Tigo Pesa Mastercard Virtual Card Number, kwa sasa inaruhusu watumiaji wa Tigo kufanya malipo kwa urahisi katika eneo lolote la ununuzi mtandaoni bila kuhitaji akaunti ya benki au kadi ya mkopo.

Ubia huo utawawezesha wafanyabiashara watatu wakubwa wa sekta ya mawasiliano kuleta mapinduzi katika mfumo wa ikolojia wa malipo ya kidijitali kwa kuwezesha malipo ya mtandaoni kwa urahisi duniani kote kupitia huduma hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Selcom, Sameer Hirji, akizungumza hivi karibuni, alisema ushirikiano huo wa kibiashara ni muhimu kwa sababu unachukua jukumu muhimu kwa ukuaji wa kampuni.

"Selcom tunajivunia dhamira yetu isiyoyumba ya ubunifu na ubora katika sekta ya malipo. Tunayofuraha kuungana na washirika kama Tigo Pesa na Mastercard kuzindua kadi yetu ya hali ya juu iliyounganishwa na pochi ya pesa ya rununu," alisema.

Makamu wa Rais Mwandamizi, Ushirikiano wa Kidijitali EEMEA Mastercard, Ngozi Megwa, alisema: "Mtazamo wetu wa ubunifu unalenga kuwezesha mabadiliko ya kidijitali ya washirika wetu ili mamilioni ya wateja waweze kufurahia ufikiaji wa mfumoikolojia wa malipo ya kimataifa na uzoefu bora wa mtumiaji."

Alisema teknolojia imetayarishwa kikamilifu ili kuwawezesha washirika wao kuzindua usuluhisho bunifu na yanayofaa ambayo yataunda pendekezo dhabiti la thamani kwa wateja wao wote.

Kwa uhusiano wetu ulioimarika na wahusika wa sekta ya mawasiliano ya simu, ushirikiano huu na Tigo unajumuisha dhamira ya kupanua zaidi chaguo la wateja na ufikiaji wa biashara ya kidijitali.

# Chupa 44 damu zakusanywa kwa upasuaji moyo

**Na Joseph Mwendapole**

CHUPA 44 za damu zimekusanywa katika uchangiaji damu kwa ajili ya watoto watakaofanyiwa upasuaji wakati wa kambi maalum itakayofanywa na wataalam wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Kwenye kambi hiyo, JKCI itashirikiana na madaktari kutoka mradi wa Little Heart wa Shirika la Muntada Aid lenye makao yake makuu Londo, Uingereza. Kambi hiyo iliyoanza juzi, itamalizika Ijumaa ijayo jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia uchangiaji damu, Daktari bingwa wa upasuaji wa moyo kwa watoto wa JKCI, Godwin Sharau, alisema uhitaji wa damu katika upasuaji wa moyo kwa watoto ni mkubwa kwa kuwa mtoto mmoja anaweza kutumia chupa mbili mpaka nne za damu.

"Upasuaji wa moyo unahitaji damu nyingi sana kwa sababu baadhi ya damu hutumika katika mashine inayosambaza damu kwa mgonjwa wakati wa upasuaji na damu nyingine uandaliwa kwa ajili ya dharura pale ambapo damu itahitajika", alisema Dk. Godwin.

Katibu Mkuu wa taasisi inayojihusisha na huduma za kijamii ikiwemo na kuchangia damu ya JAI, Saad Salim, alisema kuchangia damu ni moja ya utaratibu wa kikundi hicho kwani wanafahamu ya kwamba damu uhai na uhitajika kwa wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji.

"Huu ni utaratibu wa kikundi chetu kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wengine. Kwa hapa JKCI hii ni mara yetu ya pili kuchangia damu, mara ya kwanza tulichangia damu mwaka 2015 ambapo kupitia Taasisi yetu uniti 35 za damu zilipatikana," alisema.

Salim alisema jamii inatakiwa kuona umuhimu wa kujitokeza kuchangia damu pale huduma hiyo inapohitajika mahospitalini kwani kuokoa maisha ya mgonjwa anayehitaji damu ni thawabu.

"Jamii itambue kwamba mahitaji ya damu ni makubwa hivyo inatakiwa kuweka utaratibu wa kuchangia damu katika mahospitali yetu kwani unapochangia damu inakwenda kuwasaidia wananchi wengine ambao nao wanatamani kuwa na afya kama sisi tulivyo", alisisitiza.

Naye Ofisa Uhamasishaji Kanda ya Mashariki kutoka Mpango wa Taifa wa Damu Salamu, Mary Meshy, alisema mwitikio wa wananchi kuchangia damu umekuwa mkubwa kwa kiasi chake lakini jamii bado inapaswa kutambua ya kwamba damu haijawahi kutosha hivyo waendelee kuchangia ili kuweza kuokoa maisha ya wengine.

"Watu wengi wameguswa na kufika hapa JKCI kwa ajili ya kuchangia damu ila bado uhitaji wa damu ni mkubwa, anayepaswa kuchangia damu kwa mwanamke asiwe mjamzito wala anayenyonyesha na asiwe na magonjwa yoyote hasa yale ya kurithi", alisisitiza.

Mwanafunzi wa chuo cha Paradigms kilichoko Kimara, Dar es Salaam, Denis Mziba, alisema wanachuo wenzake kutoka chuo hicho wameona umuhimu wa kushiriki uchangiaji damu kuwasaidia watoto wanaohitaji kufanyiwa upasuaji wa moyo.

"Nimeona umuhimu wa mimi na wenzangu wenzangu kuchangia damu ili kuweza kufanikisha matibabu ya upasuaji wa moyo kwa watoto wanaotibiwa hapa JKCI na tunaahidi tutaendelea kufanya hivi kila wakati," alisema Denis.



Mbunge mstaafu wa jimbo la Muheza, mkoani Tanga, Hebert Mntangi akichimba mtaro wa msingi wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa ofisi mpya ya CCM ya wilaya hiyo, itakayokuwa ya ghorofa katika Kata ya Genge jana. Wengine ni Mwenyekiti wa CCM wilaya hiyo, Laick Gugu (kulia), Katibu wa CCM wilaya, Simon Leng'ese (wanne kulia) na (watano kushoto) ni Katibu Tawala wilaya hiyo, Desderia Haule. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kituo kipya cha afya Chuma kuwaondolea kero wagonjwa

**Na Romana Mallya**

ZAIDI ya wakazi 14,000 wa kata ya Chuma, Kilwa mkoani Lindi, sasa watapata huduma za afya bila kutembea umbali mrefu baada ya kituo cha afya kilichokuwa kinajengwa kukamilika na kukabidhiwa rasmi.

Kituo hicho ambacho kimejengwa kwa gharama ya Dola za Marekani 380,000 (zaidi ya Sh. milioni 800) chini ya Kampuni ya PanAfrican Energy Limited (PAET), kimekabidhiwa rasmi kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Christopher Ngubiagai , kwa ajili ya kuanza kutoa huduma.

Akizungumza wakati wa kukabidhi kituo hicho, Meneja wa Uwajibikaji kwa Jamii wa PAET, Andrew Kashangaki, alisema kituo hicho kitatoa huduma za haraka kwa jamii.

"Kinajumuisha idara ya wagonjwa wa nje, wodi za wazazi, ukumbi wa upasuaji, maabara, chumba cha kuhifadhia maiti na cha kuhifadhia nguo," alisema.

Alisema wanajivunia jukumu lao Tanzania na kituo hicho ni udhibitisho wa kutoa mchango chanya kwa jamii katika eneo hilo.

Pia alisema kituo hicho kitapunguza mzigo kwa vituo vya afya vya mjini ikiwamo msongamano na hivyo kuboresha ubora wa huduma kwa wagonjwa wote.

Akizungumza baada ya kupokea majengo hayo, Ngubiagai alisisitiza dhamira ya serikali ya kutoa huduma bora za afya kwa wakazi wa Kilwa.

Kiongozi huyo aliishukuru kampuni hiyo kwa mradi huo ambao utahakikisha wananchi wanapata huduma za kijamii zikiwamo za afya.

"Ninakumbuka nilipofika Chumo kwa mara ya kwanza, malalamiko makubwa niliyoyasikia ni ukosefu wa vituo vya kutolea huduma za afya.

Tarafa ya Kipatimo ina kata tano ambazo zote zinategemea kijiji cha Kipatimo ambacho kiko umbali mrefu sana hasa ikizingatiwa kuwa usafiri ni mgumu.

"Kwa hiyo nilizungumza na washirika wetu wa PanAfrican kuwaambia kuhusu matatizo wanayokumbana nayo wakazi wa Chumo, walielewa na walianza mpango wa kituo hiki mwaka 2017 na hapa tupo leo tukiwa na majengo kamili yenye thamani ya zaidi ya Sh.milioni 800," alisema.

Ngubiagai aliwashukuru baadhi ya wakazi wa Chumo waliotoa ardhi kwa jamii kujenga kituo ambacho kitakachotoa huduma kwa watoto, wajawazito, wazee na makundi mengine.

# MAISHA

MEI 14, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*


Ukurasa 14




## JUICE YA KAROTI, TANGAWIZI, NDIMU

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



## Haya ndiyo magonjwa hatari kwenye nyumba




## KATUNIKA


Ukurasa 16

# Fanya hivi kuondoa makunyanzi usoni



Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



17635484762 3
173687483492
945839428578
485938953848
209428948429

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| N | ■ | W | A | N | G | A |
| Y | ■ | ■ | ■ | Y | ■ | M |
| O | ■ | M | F | U | ■ | I |
| O | F | A | ■ | T | I | N |
| S | ■ | M | T | I | ■ | I |
| H | ■ | B | ■ | ■ | ■ | K |
| A | S | A | L | I | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


KOO, KAA, DUA, TIA, DAKWA, BWATO
INAMA, UMBWA, SHAKANI, AKWATUE

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

MALIZIA MCHORO HUU KWA KUUNGANISHA NUKTA KUTOKA NAMBA 1 MPAKA 23




# WATOTO

## PAKA RANGI



@ A.MSAMBA

## CHEKA

SHUHUDIA jinsi mgambo walipokwenda kumkamata jamaa mmoja

**Mgambo:** Hodi, hodi
**Jamaa:** Kimya
**Mgambo:** Hodi, hodi wenye nyumbaa
**Jamaa:** We nani kwani?
**Mgambo:** Sisi mgambo
**Jamaa:** Sawa, mnataka nini?
**Mgambo:** Kuongea na wewe
**Jamaa:** Kuongea na mimi?!
**Mgambo:** Ndio
**Jamaa:** Mko wangapi?
**Mgambo:** Watatu
**Jamaa:** Kama mko watatu si muongee wenyewe...!!!

**SWALI**

Paka ana manufaa gani kwa binadamu?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Ndoa ya kulazimisha, sasa kaniacha eti hawaoi kwetu!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kujadili yanayojiri kwenye anga la familia zetu kila uchao. Ni mengi na ukisimuliwa unabaki mdomo wazi na kujiuliza chimbuko la haya yote ni kitu gani?

Wiki iliyopita nilieleza kituko cha dada mmoja alienda kwao kwa maelezo kuwa aliitwa na mama yake kwenda kumuuguza. Mume akamruhusu akaenda na watoto wawili wadogo.

Miezi miwili baadaye mume kumfuatilia arudi akadai bado anauguza. Ilipojiri miezi minne ikabidi amfuate huko kwao Geita. Kumbe mama alishapona na cha ajabu bibie alikuwa na mimba ya miezi mitatu.

Jamaa kumbana akakiri ni kweli ana mimba, jamaa wa pale kijijini kwao. Kuona vile akamwambia aendelee naye ila watoto wabaki na bibi atawasomesha na kuwatunza hapo. Mahusiano yakaishia hapo.

Mpenzi msomaji wangu hayo ndiyo maisha wengine wanayotafuta duniani hapa. Hebu sikia na kituko hiki kingine. Dada mmoja akanitumia ujumbe mfupi simu ya kiganjani akisema hivi;- "Dada huwa nasoma sana habari zako. Mimi pia ni mhanga kwenye ndoa. Nimeachwa na watoto wawili tangu 2017 ikiwa sababu ni misemo ya kwao kwamba wanaoana wenyewe kwa wenyewe."

Mwanamke huyu akisimulia mkasa wake anasema ana watoto wawili wa kiume, mkubwa umri wa miaka 11 na mdogo miaka sita. Alifunga ndoa mwaka 2013 baada tu ya kumzaa mtoto wa kwanza.

Hata hivyo, ilijitokeza sintofahamu walipoamua kufunga ndoa kwani wazazi wa pande zote mbili hawakushiriki. Walionekana kususia tukio hilo japokuwa lilifanyika kwa kulazimisha.

Waliendelea na maisha bila msuguano wowote. Mume ni fundi ujenzi na mwanamke ni fundi cherehani akishona nguo za aina mbalimbali.

Matatizo yalianza pale mume alipoondoka kwenda kwao kwa maelezo kwamba ameitwa kwenda kukabidhiwa shamba. Hiyo ilikuwa ni mwaka 2017. Akaondoka kwenda huko kwao mkoani ambako alikaa kwa muda.

Aliporudi Dar akaanza kunifanyia vituko kwamba hawezi kuishi tena na mimi, kwani ukoo wao hauruhusiwi kuoa mwanamke kutoka ukoo wetu. Ndipo akaondoka hakurejea tena kwangu.

Nilijaribu mara kadhaa kwenda kumfuatilia kwao lakini niliambulia kutukanwa na kufukuzwa pamoja na watoto wangu. Hata mjomba wake akanitamkia wazi kwamba nisikanyage tena kwao kwani wao hawaoi kwetu.

Tokea wakati huo nimekuwa napambana na maisha kutunza watoto wangu mwenyewe. Namshukuru sana Mungu wote wapo shuleni. Naamini Mungu yupo pamoja nami na atanishindia mapito haya yote.

Mpenzi msomaji, bila shaka umemsikia mwenzetu huyo kwa yale anayopitia katika maisha yake. Ni muhimu tuelewe kwamba maisha ni mtiririko wa matukio, mabaya na pia mazuri.

Anayopitia mama huyu yalinipa kuwaza sana. Lakini nikajielekeza katika maeneo kadhaa yanayoweza kuwa chanzo cha haya anayopitia. Hakuna kinachotokea kwa bahati mbaya, lazima kipo chanzo au nisema asili fulani iliyosimama.

Kwanza ukiona tatizo lipo leo, rudi nyuma uchunguze mwanzo wako ulikuwaje. Wawili hawa walilazimisha kuzaa kwanza ndipo wakaoana. Pia ndoa yao ilikuwa ya kulazimisha kwani wazazi pande zote mbili hawakushiriki. Tayari ni ndoa iliyokataliwa.

Wakaendelea na maisha. Roho ya kukataliwa kwa mwanamke huyu ikajitokeza tena baadaye. Upande wa kijana ukainuka na kumwambia bibie kwamba walikosea kumuoa kwani ukoo wao hawaoani na ukoo wao. Ama kweli Maisha ndivyo Yalivyo!

Jambo lingine ninaloliona ni pale kijana alipoitwa kukabidhiwa shamba. Inawezekana ni shamba kweli kama ambavyo mila zao zinataka kurithishwa ardhi zilizoasisiwa na mababu. Au wengine waabudu mizimu hadi leo yawezekana aliende kukabidhiwa mikoba ya familia au ukoo.

Huko anakotoka kijana bado wengi wanaabudu miungu kwa maana ya kuendekeza matambiko. Kila wafanyacho wanawasilikiza mizimu ya kwao. Siyo ajabu ndiyo hiyo mizimu iliyomwamuru kijana kumuacha mwanamke huyo.

Bibie akaniambia kwamba pale alipoamua kuingia kwenye wokovu na kutafuta nguvu ya Mungu kwa bidii, ndivyo mumewe alivyokuwa akimkasirikia kwamba hataki aende kwenye makanisa ya waokovu.

Hivi sasa mama huyo amepiga moyo konde na kuelekeza hatua zake kutafuta nguvu ya Mungu kwa maombi, akiamini kwamba Mungu ndiye aliye juu ya vyote naye ni msaada wa wote wamkimbiliao. Niishie hapa. Hakika Maisha ndivyo Yalivyo. **Je, una kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# TSB uko wapi utafiti mikoa mipya inayofaa kustawisha mkonge?

KUTOKANA na mabadiliko makubwa ya tabianchi kwa sasa, wakulima wengi wamekuwa wakikosa mavuno kutokana na kutegemea mvua ambazo kwa sasa mtiririko wake si mzuri.

Katika hali hiyo, watafiti wa mkonge, wameanza kuhamasisha kilimo cha zao hilo kwa wakulima wadogo nchi nzima ili kitumike kuwaongezea kipato kwa kuwa linavumilia ukame. Halina msimu maalumu wa kupanda na halina wakati maalumu wa kuvunwa pale linapokuwa tayari kuvunwa.

Kimsingi, mkonge unaweza kuchanganywa na mazao mengine ya msimu kama kunde, mahindi, maharage, alizeti, njegere na karanga kwa vile ni zao ambalo halina uhaba wa vipando.

Kama bidhaa zitokanazo na mkonge zinaweza kutumika katika sekta ya kilimo, nishati, ujenzi, famasia, magari, meli, nyumbani, ofisini na mazingira mengine, najiuliza kuna utafiti umefanyika ili kubaini mikoa mipya inayoweza kulima au kustawisha mkonge nchini, ukiachana na ile ya wakulima wadogo katika wilaya za Muheza, Korogwe, Handeni, Kilosa, Mkinga, Singida, Tarime, Bunda, Rorya, Mkuranga, Rufiji, Ruangwa, Bariadi, Shinyanga na Same?

Kwa nini basi Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB) hadi sasa haijatangaza inafanya utafiti maeneo gani nchini ili kuendelea kuhamasisha kilimo hicho kama ilivyo kwa mazao mengine ya kimkakati ambayo serikali imekuwa ikifanya hivyo?

Kwa nini mashamba ya wakulima wadogo, yanayomilikiwa na vyama vya ushirika, yasifanyiwe utafiti kama yanafaa kuzalisha mkonge yakatumika kuwafuta machozi Watanzania, badala ya kuwaacha wakaendelea kung'ang'ania kulima mazao kama mahindi na wasipate tija katika mavuno?

Hivi lile agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuzitaka halmashauri zinazozalisha mkonge, kuanzisha vitalu vya kuzalisha miche bora ya mkonge na kuigawa kwa wakulima ili kufufua mashamba zaidi na kuongeza uzalishaji zao la mkonge nchini limetekelezwa kwa asilimia ngapi? Nauliza hilo kwa sababu nakumbuka Majaliwa aliwahi kusema mkakati wa serikali ni kuhakikisha wakulima wadogo na wakubwa wanasukumwa kufufua mashamba yao ya mkonge ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo muhimu nchini.

Tunajua mmea wa mkonge unaweza kuishi kwa kipindi cha miaka 10 hadi 25. Kama ndivyo, kwa nini TSB haijaanzisha kampeni ya hamasa kuwaamsha Watanzania kuchangamkia fursa hiyo ya kilimo cha mkonge ili kumhakikishia mkulima kipato cha uhakika?

Taarifa za kitaalam zinaonyesha mkonge ni zao linalostahimili magonjwa, wadudu na magugu na hata upungufu wa rutuba kwenye udongo. Ni wakati mwafaka sasa, serikali kusambaza bure miche ya mkonge kwa wakulima katika mikoa inayofaa kustawisha zao hilo.

Walau Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ametupa mwanga kwamba serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Mlingano, mwaka ujao wa fedha itaanza ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche ya mkonge kwa njia ya chupa. Lakini pia kuna uhifadhi wa mbegu za asili na TARI-Mlingano, imeendelea kutunza vinasaba 60 vya mkonge.

Kwamba hadi Aprili, mwaka huu, TSB imesambaza miche milioni 12.6 katika halmashauri 15 nchini. Ni jambo jema kwa kuwa tunalenga kuwainua wakulima wadogo nchini.

Kanzidata ya Wizara ya Kilimo, inaonyesha kwa mwaka 2020/21 tani 36,170 za mkonge zilizalishwa nchini, 2021/22 (tani 44.151) na mwaka 2022/23 tani 48,262.99.

Si haba kwa kuwa hadi kufikia Aprili mwaka huu, uzalishaji wa singa za mkonge umefikia tani 48,262.99, sawa na asilimia 80.4 ya lengo la kuzalisha tani 60,000; na vilevile TSB, imetoa mafunzo ya kilimo bora cha mkonge kwa wakulima wadogo 3,952 na wakulima wakubwa 17 ikilinganishwa na lengo la kuwafikia wakulima 8,000.

Ni faraja kusikia, nchi yetu imefanikiwa kuwaunganisha wakulima 2,500 na soko kwa mfumo wa zabuni, ikilinganishwa na lengo la wakulima 2,400 waliokusudiwa; wakati uzalishaji wa mkonge utaongezeka kutoka tani 48,263 mwaka 2022/2023 hadi tani 60,000 mwaka 2023/24.

Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. ***Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***







ILIKUWA SIKU YA FURAHA KWA BWANA HAMZA VEDASTUS NA BI. IRENE MIJAI, WALIPOFUNGA NDOA TAKATIFU MEI 7, MWAKA HUU KATIKA KANISA LA WASABATO TABATA CHANG'OMBE, WILAYANI ILALA JIJINI DAR ES SALAAM NA BAADAYE KUFUATIWA NA TAFRIJA FUPI.





# MITINDO

Na Mary Geofrey



# Kuwa mjanja tupia kivazi na raba sneakers

MIAKA iliyopita sneakers (raba) zilikuwa zinatumika zaidi kwenye kufanyia mazoezi.

Mambo yamebadilika. Sneakers zinaweza kuvaliwa kwenye outfit na ukaonekana nadhifu.

Wakati wa majira ya joto utagundua kwamba sneakers zimekuwa miongoni mwa vitu vinavyovaliwa zaidi hususani kwenye mitoko ya kawaida.

Wanawake nao wanashika hatamu siku hizi kwenye sneakers hasa mabinti ambao wanakwenda na 'fashion'.

Kwa wale wanaotamani kutoka wakiwa 'simple but stylish' unaweza kujaribu kuvaa 'outfit' na sneaker.

Wabunifu kama Giuseppe,Adidas, Converse wapo mstari wa mbele kutengeneza sneakers kwa ajili ya wanawake ambazo zinatumika kama vivazi nje ya mazoezi.

Unaweza kuvaa sneakers na aina nyingi za nguo kuanzia sketi, jeans, kaptula na hata magauni ya maxi kama ambavyo unaona kwenye picha.





## UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# Fanya hivi kuondoa makunyanzi usoni

MIKUNJO ni moja ya ishara ya wazi ya kuzeeka. Ndio sababu wataalam wa urembo wanashauri kutunza ngozi yako wakati wa ujana.

Vijana hawana alama za mikunjo kwa sababu muda wake bado inajitokeza wakati ambao umri wako umeanza kusogea.

Kuna mambo mengi ambayo yanaweza kuathiri kuonekana kwa makunyanzi na lazima izingatiwe. Pia, kuna njia kadhaa za kulainisha au kuondoa mikunjo ya kwanza.

Njia moja bora ya kuzuia mikunjo ni kutunza ngozi kwa kiwango cha juu.

Wakati wa ujana hakikisha unatunza ngozi yako ya uso kwa kuzingatia kuwa na unyevu unyevu na kuzuia uchafu.

Ikiwa ngozi ina mafuta, unapaswa kusafishwa na bidhaa ambazo sio za kemikali na kuongeza unyevu kwa maji.

Kwa hali yoyote, ngozi ya mafuta huwa na mikunjo michache tofauti na ngozi iliyokavu ambayo inakuwa rahisi kujaa mikunjo.

Tumia mafuta ya asili

Kwa wale ambao tayari ngozi zao zimeanza kuwa na mikunjo, njia rahisi na salama kuiondoa ni kutumia mafuta ya asili.

Mafuta ya asili ni msaada mzuri wa kuondoa mistari na mikunjo inayoonekana usoni.

Unaweza kutumia mafuta kama nazi, jojoba, ambayo ni sawa na mafuta yayozalishwa na ngozi, au ile ya mlozi, ambayo pia ni ya kiuchumi sana.

Mafuta ya komamanga na mafuta ya rosehip yanapendekezwa haswa kwa mikunjo.

Unaweza kutumia tu matone machache katika maeneo ambayo kawaida kasoro huonekana.

Epuka mafuta katika maeneo ambayo una mafuta kwa sababu uchafu zaidi unaweza kuonekana.



## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Juice ya karoti, tangawizi, ndimu

JUISI ya karoti na tangawizi ni rahisi kutengeneza na ina faida kubwa sana katika mwili wa binadamu na cha kushangaza zaidi ni tamu.

Juisi hii itabadilisha kabisa mwonekano wako wa ngozi pia mwili kuwa na joto la kutosha hasa kuzingatia kipindi hiki cha baridi kali na sio wale walio katika ukanda wa joto wasitumie la hasha hutumiwa sehemu yoyote.

**Mahitaji**

Tangawizi kiasi cha usawa wa kiganja chako, karoti nusu kilo na ndimu tatu.

Namna ya kuandaa

Unaweza kuanza kwa kumenya tangawizi, karoti zako na kusafisha ila iweke kwenye chombo safi.

Anza kusaga tangawizi peke yake kwa kutumia brenda au kikwaruzo cha kawaida kisha ichuje na kuweka kwenye chombo kisafi.

Baada ya hapo chukua karoti zako na anza kuzisaga kwa kutumia Brenda mpaka zilainike na kisha changanya na juisi ya tangawizi na ndimu, ongeza sukari kidogo na hapo itakuwa tayari kwa kunywa wakati wowote baada au kabla ya kula.







MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Haya ndiyo magonjwa hatari kwenye nyumba

KAMA ilivyo kwa viumbe hai kuathiriwa na mazingira wanayoishi, ndivyo ilivyo pia kwa viumbe visivyo hai ikiwamo nyumba.

Ili kuepuka majengo yasiathirike, ni vyema ubunifu wake ufanyike katika hali ya ubora wa hali ya juu katika sehemu husika linapojengwa jengo.

Msanifu majengo, Deodatus Kwivilo, anasema hata ujenge nyumba nzuri na kubwa kiasi gani, kama haijabuniwa na kujengwa kwa kuzingatia mazingira ya eneo husika, lazima iwe hatarini kuathirika.

Kwivilo anasema kabla ya kuanza kujenga nyumba, ni lazima ufanye uchunguzi katika eneo husika kubaini endapo kuna magonjwa yanayoweza kuathiri nyumba yako na kufanya ubunifu wa kukabiliana nayo.

Mtaalam huyo anasema endapo nyumba hiyo itajengwa pasipo kufanyiwa ubunifu mzuri, huenda ikaathiriwa na magonjwa hayo.

Anasema miongoni mwa magonjwa yanayoathiri nyumba endapo haijafanyiwa ubunifu mzuri ni kutitia.

Mara nyingi nyumba hutitia kutokana na aina tofauti za udongo, kiwanja



au kimo cha msawazo wa msingi kuwa tofauti pamoja na ubunifu hafifu wa udongo kulingana na uzito wa jengo husika.

Ugonjwa mwingine, anasema ni nyumba kupitisha maji na kwamba maeneo mengi ya Tanzania yamezungukwa na vyanzo vya maji ambayo yanahitaji usanifu na ubunifu wa hali ya juu wakati wa ujenzi wa nyumba ili kuepuka athari baadaye.

"Maeneo mengi ya Pwani majengo yake mengi yameathiriwa na tatizo hili na hata imekuwa kero kwa wakazi na watumiaji wa majengo hayo. Baadhi ya majengo yanapitisha maji kwa njia ya sakafu na kuta mithili ya chujio au chemchem na mara nyingi utagundua kwa kuona ardhi yake inatoa maji wakati wote wa majira ya mwaka.

" Na majengo mengi ya maeneo haya yanaoza na kutitia kwa haraka na hata mashimo ya vyoo vyake huinuka kwenda juu ambalo ni hatari kwa afya za wakazi. Katika hali hii kuta na sakafu huoza kwa haraka kutokana na maji yaliyopo chini ya ardhi kuwa na kemikali mbalimbali zilizopo kwenye maji hayo. Kwa hiyo katika mazingira haya lazima yatumike malighafi sahihi za kuzuia maji hasa wakati wa ujenzi," anasema.

Lingine, anasema ni kuoza kwa nyumba na kwamba hali hiyo hutokana na unyevunyevu na kemikali mbalimbali kupitia maji kukaa kwa muda mrefu kwenye kuta na kuathiri ubora wa kuta hizo.

"Na hii husababisha kumea kwa mimea ambayo kusababisha ukungu wa kijani kwenye kuta ambao huzalisha fangasi mbalimbali wanaokula kuta," anasisitiza.

# Usilichukulie poa bafu lako

**Na Restuta James**

UNAANZA na kumalizia siku yako bafuni. Ndiyo maana wataalamu wa mapambo wanashauri kwamba hiki ni chumba kinachopaswa kuwa na mazingira ya 'anasa' na ya kifahari sana.

Ili kukifanya chumba hiki kivutie, wanashauri uweke marumaru nusu ukuta ili iwe rahisi kubadilisha mwonekano pale unapohitaji kufanya hivyo.

Hata hivyo, kwa wale ambao wameweka marumaru ukuta mzima, siyo tatizo sana kwani kuna namna nzuri ya kupendezesha bafu na choo chako.

Wataalamu wanaeleza kuwa kwa ukuta wenye marumaru nusu, chagua rangi tatu lakini moja ipakwe eneo la asilimia 70, ya pili ipakwe asilimia 20 na nyingine asilimia 10.

"Sheria ya rangi tatu inakuwezesha kuunda ufahari ambao ni vigumu kukosa kuifurahia bafu yako," inasema sehemu ya taarifa ya wataalamu hao.

Wanaeleza kuwa mabafu na vyoo ni miongoni mwa vyumba vigumu kupamba kwa sababu ya vifaa vingi visivyohamishika kama makabati na masinki, lakini unaweza kubadili mwonekano wa eneo dogo kadiri inavyowezekana.

Kwa wanaotaka kubadili mwonekano wa rangi, kijani kisichokolea ni rangi maarufu ya bafuni mwaka huu kwa sababu inatoa mandhari ya kutuliza na kuburudisha akili.


Rangi hii inaweza kutawala kwa asilimia 70, chokaa ikawa kwa asilimia 20 na asilimia 10 ikawa ya mzeituni.

"Kwa mwonekano wa kifahari, unaweza kupaka chumba kizima rangi ya kijani kisichokolea," wanashauri.

Inaelezwa zaidi kwamba rangi ya bluu tulivu, imekuwa mashuhuri kwa ajili ya chooni kwa miongo kadhaa kutokana na uwezo wake wa kuleta utulivu na mvuto.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
'UDAMBWIDAMBWI'
JUKWAANI
NGEBE KWISHA!
SHIRIKISHO NI KAMA ULINZI SHIRIKISHI HAINIUMI! ILOOOO!
MIMI KAZI YOYOTE UTAKAYONIPA NAFANYA...LAKINI NAYOIPENDA SANA KUBOMOA
NDOA YANGU INA UFA LAKINI WEWE HUNIFAI
EEEEE BABA!
'KAONA HUKU HASIKIKI!'
VUA BASI UFUE! MANAKE HAZITOKI MWILINI UTADHANI ZIMESHONEWA HUMO HUMO!
HIZI HAZIVUKI MPAKA NABEBA "JAGI" KWANI INAKUKERA?
MUME WANGU UNANIONEA WIVU AU UNANIONEA GERE?
NA MIMI KUNA KABINTI KANANIPIGIA MISELE NILIKUWA NAKARINGIA...
ENZI ZANGU SIKUWAHI KUWA NA RAFIKI ALAFU NIKAMUACHA SALAMA MKEWE
EMBU RUDIA TENA SENTENSI YAKO!
RAHA UTAMU UTAMU TUUU
USIFIKIRI SIFA MISHAVU IKIPASUKA SEWAHAJI INAKUHUSU NA HATUJI KUKUONA
...KINYUNYIZO CHA LEO...
'USIPOMSIFU MKEO WENZAKO WATAMSIFU'

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaiomba radhi Afrika Kusini

**CAPE TOWN,** AFRIKA KUSINI
WIZARA ya Mambo ya Nje ya Afrika Kusini imesema balozi wa Marekani nchini humo, Reuben Brigety ameomba radhi kwa kudai kuwa nchi hiyo iliiuzia Russia silaha.

Siku mbili zilizopita balozi wa Marekani nchini Afrika Kusini Brigety alidai kuwa meli ya Russia ilikuwa imesheheni risasi na silaha zilizotolewa na Afrika Kusini Desemba 2022. Afrika Kusini inasema haina rekodi ya mauzo ya silaha, huku Rais Cyril Ramaphosa akiagiza uchunguzi ufanyike.

Aidha, inaelezwa kuwa msemaji wa masuala ya usalama wa taifa wa Ikulu ya White House, John Kirby, hakusema lolote kuhusu maelezo ya madai hayo.

Ilielezwa kuwa Kirby alisema suala hilo ni zito na Marekani imekuwa ikizitaka nchi mara kwa mara kutounga mkono vita vya Russia nchini Ukraine.

Akiandika kwenye mitandao ya kijamii baada ya kukutana na wizara ya mambo ya nje, Brigety alisema anashukuru kwa fursa ya kurekebisha maoni yoyote potofu yaliyotokana na matamshi yake hadharani. "Tuendeleze uwepo wa ushirikiano mkubwa kati ya nchi zetu mbili na ajenda muhimu ambayo marais wetu wametupa," alisema.

Wakati huo huo waziri wa baraza la mawaziri la Afrika Kusini alikosoa akisema diplomasia ya aina hiyo Afrika Kusini haiwezi kuonewa na Marekani.

**BBC**



Maofisa wa usalama na wachunguzi wa maiti wakiwa wamebeba miili baada ya kuifukua katika msitu wa Shakahola. **PICHA: REUTERS.**

# Miili mingine 29 yafukuliwa katika msitu wa Shakahola

**NAIROBI,** KENYA
WACHUNGUZI nchini Kenya wamefukua miili mingine 29 na kufanya idadi ya waathirika wanaohusishwa na ibada ya kutokula hadi kufa ili wakutane na Yesu kufikia 179, na kwamba wengi wao ni watoto.

Polisi ilisema wanaamini kwamba miili mingi iliyopatikana katika msitu karibu na mji wa pwani wa Malindi, ulioko Bahari ya Hindi, ni wafuasi wa mchungaji Paul Mackenzie.

Inaelezwa kuwa mvua kubwa iliyokuwa ikinyesha nchini Kenya ilichelewesha operesheni ya kuchimba makaburi wiki iliyopita, na kwamba baada ya kutulia maofisa wa uchunguzi ameanza tena shughuli ya ufukuaji wa makaburi hayo.

Aidha, taarifa za polisi zinaeleza kwamba watu takribani 25 pamoja na Mackenzie wako chini ya ulinzi wa polisi na genge la watekelezaji waliopewa jukumu la kuhakikisha kuwa hakuna mtu aliyeacha kufunga au kuondoka mafichoni ndani ya msitu huo akiwa hai.

Pia taarifa zilisema Mackenzie bado hajatakiwa kujibu mashitaka, lakini mahakama iliamuru Jumatano azuiliwe kwa wiki tatu nyingine wakisubiri uchunguzi zaidi kuhusu kile kinachoitwa mauaji ya msitu wa Shakahola.

Mwanzilishi huyo wa Kanisa la Good News International mwenye umri wa miaka 50 alijisalimisha Aprili 14, mwaka huu, baada ya polisi kuanza kutilia shaka na kuingia katika msitu wa Shakahola.

Ingawa njaa inaonekana kuwa sababu kubwa ya vifo hivyo, baadhi ya waathirika wakiwemo watoto vipimo vilibaini kuwa walinyongwa, kupigwa au kuzibwa hewa, kwa mujibu wa daktari mkuu wa serikali Johansen Oduor.

Taarifa zilisema nyaraka zilizowasilishwa mahakamani mwanzoni mwa wiki hii zilisema baadhi ya maiti zilikuwa zimeondolewa viungo vyao, huku polisi wakidai washukiwa walikuwa wakihusishwa kwa lazima katika uvunaji wa viungo vyao.

Waziri wa Mambo ya Ndani Kithure Kindiki, alisisitiza kuwepo na tahadhari, na kwamba hiyo ni nadharia wanayochunguza.

Mchungaji mwingine anayetuhumiwa kuhusishwa na Mackenzie pamoja na miili iliyopatikana msituni aliachiliwa kwa dhamana mahakama ilipokutana wiki iliyopita.

**VOA**

# Pande hasimu zaendelea kupigana Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN
NDEGE za kivita zimefanya hujuma kwenye mji mkuu wa Sudan, Khartoum huku mapigano ya mitaani yakiendelea bila dalili ya kupatikana mkataba wa kumaliza vita.

Hujuma hizo zimeripotiwa ikiwa ni siku moja tangu pande hasimu kukubaliana kanuni za kuwalinda raia na kuruhusu usambazwaji wa misaada ya kiutu bila vizingiti.

Inaelezwa kuwa makubaliano hayo yaliyotiwa saini Alhamisi mjini Jeddah, hayakujumuisha mkataba wa usitishaji mapigano.

Taarifa zinabainisha kuwa tangu kuzuka mapigano nchini Sudan yamesababisha vifo vya zaidi ya watu 750 na kuwalazimisha maelfu kuzikimbia nyumba zao.

Licha ya makubaliano ya mjini Jeddah, kunakofanyika mazungumzo ya kujaribu kumaliza vita, vikosi vya pande hasimu vilishambuliana katikati ya viunga vya mji mkuu, ambao ni makaazi ya zaidi ya watu milioni tano.

Shuhuda mmoja aliiambia AFP kwamba alisikia mingurumo ya ndege za kivita na milipuko ya makombora.

AFP ilisema magharibi mwa jimbo la Darfur, eneo ambalo pia limeshuhudia mapigano makali, watu walitafuta maeneo ya kujificha kutokana na mashambulizi makali ya makombora na risasi.

Wawakilishi wa majenerali wawili wanaowania madaraka ambao ni mkuu wa jeshi na kiongozi wa taifa, Abdel al-Burhan na kiongozi wa kikosi cha wanamgambo wa (RSF), Mohamed Hamdan, walikubaliana kuhakikisha misingi ya kuwalinda raia inazingatiwa. Ilielezwa kuwa Makubaliano hayo yanajumuisha pia dhamira ya kila upande ya kuruhusu kusambazwa msaada wa kiutu kwa wanaohitaji na yanatoa wito wa kurejeshwa huduma muhimu za kijamii kama maji na umeme.

Marekani na Saudi Arabia zinazoongoza juhudi za kidiplomasia za kuutatua mzozo huo, zimesema mashauriano bado yanaendelea ili kufikiwa mkataba wa kusitisha mapigano kwa siku 10 na kisha kufungua njia ya kutafuta makubaliano ya kukomesha kabisa mapigano.

Hata hivyo, wanadiplomasia wa Marekani wamekuwa wawazi juu ya vizingiti vilivyopo katika mazungumzo ya mjini Jeddah ambayo yamemaliza wiki sasa.

Mjumbe maalum wa Umoja wa Mataifa (UN) kwa Sudan Volker Perthes aliyakaribisha makubaliano ya kuruhusu usambazwaji msaada wa kiutu yaliyofikiwa baina ya pande hasimu, alieleza kuwa hatua hiyo ni ya manufaa, huku akisisitiza pande hizo kuendelea na majadiliano bila kuchoka.

Pia inaelezwa kwamba jitihada za kupatikana kwa mkataba wa kusitisha mapigano zinaelekea kuzaa matunda.

Pia UN inakadiria kwamba tangu kuanza kwa mapigano April 15, mwaka huu, takribani watu 200,000 wameikimbia Sudan.

Pia ilibainishwa kwamba wafanyakazi 18 wa huduma za msaada wa kibinadamu wameuwawa, hali iliyoyalazimisha mashirika mengi ya kimataifa kusitisha shughuli zake nchini Sudan.

Vile vile, kuna ripoti za wizi wa chakula cha msaada nchini humo, huku Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (WFP), likisema chakula cha msaada kilichoporwa au kuuzwa kimagendo kina thamani ya mamilioni ya dola.

**DW**

MAKALA

# SISI NDIO CHANZO CHA HILI



Na Magabilo Masambu

WAZAZI na jamii kwa ujumla tunawajibika kutoa malezi bora kwa watoto wetu. Malezi hayo ni pamoja na kuwapatia elimu, chakula, mavazi na makazi yakiwa ni mahitaji yao ya msingi, kama ilivyo kwa binadamu yeyote. Faida kubwa ya kuwatunza vizuri watoto, tutakapofikia wakati ambao hatuwezi kufanya chochote kwa sababu zozote zile, ukiwamo uzee, basi watoto hawa pia wageuke kutulea.

Watoto ni lulu, wengine wanasema ni tunu lakini zaidi ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu imani yetu ni kwamba tunawapata akipenda na tunawakosa akipenda pia. Kwa hiyo kitendo cha kumpata mtoto tukashindwa kumlea si tu tutakuwa tumejikosea bali tutakuwa tumemkosea pia Mungu wetu.

Kwa sasa bado tunalo tatizo la watoto wa mitaani kama wanavyoitwa. Lakini ni muhimu kufahamu kwamba mitaa haizai watoto kwa maana hiyo sisi ndio chanzo cha hili. Hakuna namna tutakwepa kulikubali hili, watoto wote hao wana wazazi pengine labda wawe wamefariki dunia lakini hata wakiwa wamefariki dunia vipi kuhusu ndugu? Tunataka kusema kwamba sisi hatukuwahi kulelewa na ndugu? Kama tumewahi tunaonaje ugumu kuwalea watoto wa ndugu zetu na kuamua kuwaacha waitwe watoto wa mitaani?

Ni kweli kwamba ziko sababu nyingi zinazosababisha watoto kuanza kutangatanga mojawapo ikiwa ni kuachana kwa wazazi wawili, mimba za utotoni, vifo vya wazazi wote wawili, ndugu kukataa kuwalea watoto wa jamaa zao, ugumu wa maisha kwa baadhi ya familia ambazo pengine zimebaki na wazee tu. Pamoja na haya yote, bado sisi ndio chanzo lazima tutafute njia ya kutatua tatizo hili sisi wenyewe.

Jambo la kuachana limekuwa kawaida siku hizi, ndoa hazidumu tena kama zamani kwa sababu tunaingia kirahisi, hivyo kutoka kirahisi pia. Hatukatai kuachana kwa sababu pengine kuna mambo hayavumiliki kwenye ndoa lakini ni muhimu kuhakikisha wakati mnaachana unakuwepo utaratibu mzuri wa malezi ya watoto ili wasichague kuingia mtaani.

Ugumu wa maisha nao ni hoja nyingine ambayo mara nyingi tukizungumza na hao watoto wataitaja kwamba nyumbani hali ngumu, ndiyo maana niko hapa mtaani naombaomba nipate fedha za kupeleka nyumbani. Ikumbukwe kwamba maisha magumu hayako kwako tu hata wengine wana maisha magumu wakati mwingine kuzidi hata uliyo nayo. Pamoja na hayo, watoto wao bado hawaingi mtaani kwa sababu kwa kufanya hivyo unafanya kizazi kizima kiwe ni cha kuombaomba na hii hatari yake ni kwamba watoto hao wasipokwenda shuleni maana yake hawatakuwa na kesho nzuri. Ni kweli kwamba watapata fedha ya kula leo lakini vipi kesho yao?

Mimba za utotoni, ni kweli kwamba kuna wakati mtoto mdogo anaweza kuzalishwa na kijana mdogo ambaye hajaweza kujitegemea. Kitu ambacho mara nyingi imetokea kukimbia hizo mimba na pale binti anapojifungua anakutana na ugumu wa kumlea mtoto mwishoe kumtelekeza. Rai yangu ni kwamba kama unaona hujawa tayari kutoa malezi kwa mtoto basi ni muhimu kujiepusha na uhusiano usio na mpango kwa sababu kesho na kesho kutwa tutaanza kumwona mtoto wako mtaani.

Wazazi kufariki dunia inaweza kuwa sababu pia. Inaweza kutokea katika umri mdogo kupotelewa na wazazi wote wawili lakini hawa wazazi hawana ndugu? Na kama wapo kwa nini wasigawane malezi ya watoto? Mara kadhaa tumeona watu wakionyesha huruma juu ya watoto wa marehemu siku za misiba lakini cha ajabu ni kwamba baada ya msiba huwa wanawatelekeza watoto wa ndugu zao na wengine walisaidiwa na hao marehemu enzi za uhai wao lakini leo baba au mama zao wanapofariki dunia, tunasahau mema yote.

Kuna baadhi ya wazazi wanaishi mijini wametelekeza watoto kwa wazazi wao (babu na bibi) vijijini huku wakitumbua raha huku mjini na wakati mwingine hakuna mawasiliano kati yao. Maisha yanapokuwa magumu watoto wanaamua kuingia mitaani na hili nalo tunasababisha sisi tulioko mijini. Tuwakumbuke wazee na watoto wetu tuliowaacha huko vijijini, tuwasaidie kwa sababu maisha tuliyo nayo mjini hayadumu. Kuna siku tutahitaji msaada wa watoto wetu hao na hatutaupata kwa sababu hatukuwaandaa kutusaidia mapema.

Serikali na wadau ni muhimu kufikiria namna bora ya kutatua jambo hili kwa sababu iko siku watoto hawa wakipata mtu akawarubuni na kuwahakikishia maisha bora, wanaweza kutumika vibaya katika kuhatarisha usalama wa nchi. Ushauri wangu ni kwamba kuna umuhimu wa kuwakusanya mahali na kuwapatia mafunzo ya ujuzi ili kuwafanya wajitegemee baadaye na kusaidia wengine. Ni watoto wetu na ni Watanzania.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Chatu Mkali' na 'MV Mapenzi' zilivyotungwa kwa lugha picha



Na Adam Fungamwango

WANAMUZIKI na wasanii wa sasa wana kazi kubwa sana ya kupambana na wa zamani ambao walifanya kazi kubwa sana licha ya kwamba teknolojia ilikuwa duni.

Ukisikiliza nyimbo za sasa hata jinsi zinavyorekodiwa tu licha ya kwamba ni ndani ya studio za kisasa kabisa lakini kiwango hakilingani na zile zilizokuwa zikirekodiwa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) tangu miaka ya 1960 hadi mwishoni mwa miaka ya 1990.

Tena walirekodi kwa njia moja tu lakini muziki wake hadi leo ukipigwa unasisimua mwili hadi akili.

Nikisema njia moja nina maana kuwa kwenye utaalam wa kurekodi nyimbo hasa za kisasa, kila chombo kinarekodiwa kinyake, halafu baadaye wimbo wote unachanganywa.

Solo, rhythm, bass, drums, saxophone, trumpet, kinanda na hata waimbaji, kila idara inarekodiwa na njia yake halafu 'prodyuza' anafanya mchanganyo wa kuziunganisha na kuwa wimbo kamili.

Ndiyo maana kwenye studio za kisasa anaweza kwenda mpiga chombo kimoja tu akaenda kurekodi, halafu wenzake wakaenda baadaye hadi siku nyingine.

Si hivyo kwa RTD zamani. Bendi zilikwenda kurekodi kama zinapiga kwenye kumbi. Wote wanalazimika kupiga pamoja na mmoja anapokosea, basi muziki wote unafutwa, hata ikiwa mara saba mpaka pale watakaporekodi kwa usahihi.

Hii ilisababisha zamani bendi ikienda kurekodi RTD, basi itashinda huko siku nzima na unaweza kukuta imerekodi nyimbo tano au sita. Lakini kuna baadhi ya bendi wanamuziki wake walikuwa makini sana, walirekodi hata nyimbo 11 kwa kipindi kifupi tu bila kurudiarudia. Hii ndiyo inaitwa kurekodi kwa njia moja.

Pamoja na yote, ule muziki iliorekodiwa kwa njia moja, hadi leo inasikika kwa uzuri sana na ina ubora kuliko hata zilizorekodiwa kwenye studio za kisasa.

Ukitaka kuthibitisha hilo, waulize wachambuzi wa muziki wa dansi, wanapopiga 'remix' ya nyimbo yoyote ile ya zamani ambayo imepigwa na bendi hiyo hiyo, lakini wakairudia baadaye kwenye studio za kisasa. Wanasikizaji wengi huwa hawazitaki 'remix' badala yake wanataka zipigwe zile zile halisi, ambazo zilirekodiwa awali RTD.

Nikitoka hapo naelekea kwenye utunzi wenyewe. Watunzi wa kisasa wamekosa ubunifu mwingi tu. Leo nitautaja mmoja. Ni kutunga nyimbo kwa lugha ya picha. Kwa sasa hakuna nyimbo kama hizo. Zamani wanamuziki waliweza sana kutunga nyumbo za kufumbafumba. Anaweza kuimba maji, lakini kumbe si hayo anayozungumza. Anazungumzia kitu kingine kabisa. Atamwimba mnyama au ndege, msikilizaji inabidi ujiongeze sana ndiyo ujue kuwa anayeimbwa na binadamu au mtu fulani. Vinginevyo 'ushikwe masikio' na mtu mwingine.

Ziko nyingi sana lakini leo nitajikita kwa nyimbo tatu. wa kwanza ni 'Mv Mapenzi' namba mbili uliopigwa na DDC Mlimani Park Orchestra miaka ya 1980. Mashairi yake ni haya hapa.

"MV mapenzi meli ya wapendanao, moyo kama bahari, manahodha mimi na wewe. Kuchafuka kwa bahari siyo wa safari. Meli ilipokumbwa na dhoruba nahodha kajitosa baharini. Wale papa na nyanguni, wenye uchu, wamemmeza ooh masikini.

"MV Mapenzi, meli ya wapendanao bendara inapepea safari yaendelea.

Mabaharia wenye upendo wameikabili dhoruba, ushirikiano na bidii ndiyo silaha yao ya kweli, na upendo ukitawala roho, kamwe hutaona machafuko moyoni mwako, kamwe hutoona kichefuchefu moyoni mwako."

Hapa utakachofikiria ni hicho kuwa bahari ilichafuka na nahodha wao wakajitosa baharini akamezwa na papa na nyangumi, lakini mabaharia wakendelea na safari yao kama ilivyopangwa.

Lakini ukweli ni kwamba baharia anayeimbwa hapo ni Muhidini Maalim Gurumo, ambaye alikuwa kiongozi wa bendi hiyo. Aliihama bendi hiyo mwaka 1985 na wenzake kwenda Orchestra Safari Sound wakaipa mtindo wa Ndekule. Wanamuziki waliobaki Sikinde, wakatunga wimbo huo kuonyesha jinsi tukio lilivyotokea, lakini walilitunga kwa lugha ya picha. Papa na Nyangumi ni mmiliki wa OSS na bendi yenyewe waliomchukua, wakaambiwa wamemeza nahodha wao.

Ndekule nao walilijibu tukio hilo vile vile kwa lugha ya picha na kuwaonya Sikinde, ingawa kwa hali ya kawaida ukiisikia huwezi ukafahamu kwa urahisi.

"Chatu Mkali porini kwa nini wamuogopa? Mnyama aisiye kivuli hana mfupa, tena jabali apitapo hana pupa, apenda machakani mjini hakuzoea.

Hutega njiani siku akikusudia, ni mwepesi kumbaini adui kumfikia, usimchezee ndugu utaangania, ukufika msukosuko ujue kuzaliwa.

Usimchezee chatu, ooh chatu we ndongo usimtupie utaukosa ushindi.

"Natoa onyo kwa yoyote anayemchezea chatu ni hatari, atakuwa asipate lolote la manufaa, na ajali imkute bila ya kutegemea, atakuja adhirika ajute na dunia."

Kwa haraka haraka unaweza kudhani anayezungumzwa hapa ni chatu mnyama. Kilichofanyika imechukuliwa taswira tu ya mnyama huyo, ujabali wake na tabia yake, akavishwa binadamu.

Gurumo na Hassan Rehani Bitchuka ambao walitoka Sikinde walikuwa wanawajibu kuwa wasiwachezee na kuwafuatafuata kwa sababu hawatapata chochote cha manufaa, badala yake wataumia tu na kushuka kimuziki. Wao ni kama chatu ambaye hatakiwi kuchezewa ovyo.

Ni kweli kabisa kuna watu ambao ni wapole, wakimya na wacheshi. Kutokana na tabia zao, wengine wanawachukulia kama ni dhaifu na hawana lolote, wanaanza kuwachokoza na kuwafanyia kila aiba ya hila mbaya. Kumbe wao ni kama chatu, pamoja upole, akikaa kiupweke na hana bughuza na mtu, lakini akichokozwa na kucharuka hapakaliki.

Tujitahidi sana kuheshimu watu ambao ni wakarimu, wapole, wanyenyekevu, tusichukulie tabia yao hiyo kuwaona ni dhaifu, kumbe hatujui upande wao wa pili, ni hatari kama chatu, atakumeza tu.

**Tuma maoni 0716 350534**

# HADITHI

# Simu ya Sumu-10

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)




SHEMEJI huu mguu unaouona ni wa kwako." Alianzisha mazungumzo na Husna alikaa kimya bila kujibu chochote akiendelea kumsikiliza kwa makini.

"Nimekuja hapa kwa lengo la kukukaribisha kwenye kijisherehe nyumbani kwangu."Ni maneno ambayo yalimshusha presha Husna, lakini ilikuwa karibu aangue kicheko.

"Shemeji bwana, yaani umetoka nyumbani kote huko kuja kunialika, halafu kitu chenyewe unasema kijisherehe kweli?" Akamuuliza, halafu sasa kile kicheko alichota kucheka mwanzo akakiachia. Belo naye ilibidi amuunge mkono, halafu akasema.

"Usicheke shemeji, sasa ukisema sherehe hapa, unaweza kudhani ya harusi, mimi naona, au sherehe kubwa, kwanza hii siyo sherehe nimekosea kiswahili ni pati tu, au naweza kusema kijipati."

"Mhh! Shemeji, haya, hicho kijipati kinasemaje na cha nini?"

"Ni cha 'bethdei' tu, binti yangu Tima anatimiza miaka mitano. Nimealika watu kadhaa, lakini pamoja na kwamba kwa sasa umetengana na mdogo wangu, bado mna mtafaruku lakini bado hamjapeana talaka, mimi nimekuja kukualika kama shemeji yangu, ukusanyike pale na wanandugu wengine kwa ajili ya pati. Na hata wifi zako wamenituma hilo."

"Kwanza mimi nashukuru kuona kumbe bado mnanikumbuka shemeji yenu. Mimi nilidhani umekuja kwa ajili ya suala la kutupatanisha na ndugu yako. Hilo kwa sasa sahau kabisa shemeji. Pia mimi sina tatizo kwa sababu mpaka kutoka huko kuja huku ina maana mnanithamini sana, lakini mimi ninachoogopa ni ugomvi!"

"Ugomvi gani tena huo shemeji?" Akashangaa Belo.

"Huyo kidudu mtu aliyenipigia simu kunitukana. Si alisema nyinyi mnamfahamu. Inawezekana wewe shemeji humfahamu, lakini dada zake wakawa wanamfahamu. Anaweza kuja baada ya kutukanana kwenye simu, sasa zikalika ngumi nyumbani kwako. Halafu shemeji, hata Dan si atakuwepo? Kutakuwa na usalama kweli, mimi na Dan hatuelewani. Halafu kwa bahati mbaya ndiyo akaja na huyo hawara yake itakuwaje?"

Belo alitabasamu, halafu akajibu. "Unajua yote haya ni dhana, hakuna aliyethibitisha, ila kama yatakuwepo basi hata huyo mwanamke wa Dan atashangaa. Ndiyo atajua kama hajui. Wewe utakuwa kama mgeni rasmi, utakaa na mimi. Hutokaa na wageni wengine waalikwa. Mke wangu upande huu wewe upande huu, hadi tafrija imalizike."

**Mtu yule alikuwa akipiga hatua moja baada ya nyingine kuelekea anakoelekea. Mtu mwingine alikuwa nyumbani kwake. Alikuwa amepigiwa simu kuwa atafika nyumbani jioni siku hiyo. Na kwa sababu siku hiyo hakuwa na kazi nyingi na mizunguko pia, alirejea nyumbani mapema kumsubiri mgeni wake.**

Husna akatabasamu. Hakutegemea majibu yale "Kumbe shemeji unanipenda eee?"

"Wewe ni shemeji yangu, na kama kuna mwanamke alikupigia simu akamwambie eti sisi ndugu zake Dan tunamtambua, ni muongo. Alitaka akurushe roho tu. Njoo kwenye pati ili huyo kidudu mtu akikuona kama alikuwa hajawahi kukuona, ajue wewe ni mwanamke wa aina gani na sisi kama ndugu tunakuchukulia vipi."

"Hapo hapo, na mimi naomba kuuliza." Ilikuwa ni sauti ya Tabia, mama mdogo wa Husna ambaye alikuwa amekaa pembeni kwa muda mrefu bila kutia neno.

Wote walimtazama na macho yao yaliongea zaidi kuliko maneno, yakimtaka aongee anachotaka kukisema.

"Mimi sikatai, na wewe mkwe umekuja kwa adabu na heshima sana kuliko ndugu yako siku ile.

Mimi nachohofia sio mnamchukua mwanangu halafu mnakwenda kumdhalilisha, au kumletea mambo yasiyo na maana huko? Sipendi, sijachoka kumlea mimi."

"Hapana mama, nimemwahidi kuwa atakuwa upande wangu. Upande ninaokaa mimi. Na hatochanganyikana na wageni wote waalikwa nyumbani kwangu. Kwanza sio wengi na wote nawafahamu, ila kama atakuja mwingine ambaye simfahamu nitakuwa macho naye sana. Halafu hata siku ya kutoka hapa kuja kwangu, nitawaletea gari kutoka kwenye haya makampuni yanayochukua abiria, nitawaelekeza waje hapa wamchukue shemeji yangu na kumleta.

Atakuwa salama salimini huko na atapata usafiri mwingine wa kumrudisha." Maneno hayo yalimfanya Husna atabasamu, mama yake alimtazama naye akatabasamu.

"Sio muende mkampige mwanangu?" Akatahadharisha, ikiwa ni mwendelezo wa kuhakikisha usalama wa binti yake.

"Atakuja na kurudi salama. Ila mama samahani nilikuwa na wazo moja. Kwa nini na wewe usijumuike mkaja wote kwenye 'bethdei' hii?"

Husna na mama yake mdogo wakatazamana tena.

"Nadhani itakuwa vizuri zaidi, utakuwa unashuhudia kila kitu. Na utakiri kuwa hakuna nia yoyote ovu, nakuomba sana, kila kitu nitafanya juu yenu."

"Sawa baba, hata mimi nimetafakari naona na mimi nije tu. Kwanza nashukuru kwa sababu umenialika, lakini pia kwa ajili ya usalama wa binti yangu na kama kila kitu kitakwenda sawa, kusema kweli litakuwa jambo la kukumbukwa sana." Tabia akasisitiza.

"Ila nachokuomba ni jambo moja."Husna akadakia. "Nini tena shemeji na wewe?"

"Sitaki mazungumzo yoyote ya muafaka na Dan. Akinisalimia na mimi nikamsalimia, hakuna tatizo, lakini sijui tukae tuyasuluhishe, hapana!" Husna akamtahadharisha shemeji yake.

"Na mimi sijawahi kuwa mpatanishi mzuri hata siku moja." Akajibu na kusababisha vicheko.

Yakaendelea mazungumzo ya hapa na pale kiasi kwamba kila mmoja alifurahi. Belo aliaga na hakuwaacha hivi hivi. Akatoa noti mbili shilingi elfu 10 na kumkabidhi shemeji yake huku mama yake mdogo akishuhudia.

"Haya shemeji nakutakia safari njema, nakuahidi tutakuja wote na mama yangu, hatutakuangusha." Husna akamuaga shemeji yake.

Alichotaka Belo kimefanikiwa. Alitaka Dan na Husna wote wahudhurie tafrija yake. Na alikwenda kuwataarifu kila mmoja kivyake.

Hakumwambia Dan kama amemualika mkewe, na wala hakumwambia Husna kama amemwalika ndugu yake. Pamoja na hayo Husna anatambua kuwa Belo na Dan ni ndugu, hivyo sio rahisi kwa mumewe kushindwa kwenda kwenye pati ya kaka yake.

Ina maana hapo ni Dan tu ndiye aliyekuwa hajui kuwa mkewe atakuwepo kwenye pati hiyo.

ITAENDELEA JUMAPILI



# KIMASOMASO, DULLA MAKABILA MSIMUONE

MIEZI mitatu tu baada ya kuingia kwenye penzi zito la binti Zainabu Said, maarufu kama ZayLissa, msanii wa nyimbo za singeli, Dulla Makabila ameamua kumchukua jumla.

Dulla amefunga ndoa juzi jijini Dar es Salaam iliyohudhuriwa na ndugu, jamaa na marafiki, huku salaam za pongezi zikiendela kumiminika.

Mwenyewe Dulla alimwagia sifa mkewe mpya, huku akisema hiyo ni ndoa ya pili kwake, lakini ya kwanza ilishavunjika kitambo.

"Sina maneno mengi, nimeonyesha upendo wangu kwa vitendo, huyu ni mwanamke wa ndoto yangu, ni muda mrefu sana nilitamani kuwa naye. Hata mwenyewe nilimwambia, nimetimiza kile nilichokipanga kwa muda mrefu.

Alipoulizwa Zaibabu ni mwanamke aina gani jamaa alifunguka jumla.

"Huyu si mwanamke wa kwanza mimi kuwa naye, lakini kilichofanya nimuoe, kuna sifa zile ambazo mimi mwenyewe nilikuwa nazitaka mwanamke nimkute nazo ndiyo nimuoe. Kikubwa amekubali kuwa mke, siyo kama ni mwanamke ambaye alihitaji tu kuwa na mume, ila yeye alijipanga kuwa mke.

Mimi kuna heshima yangu nilitaka nipate kutoka kwa mke wangu wa ndoa. Hii kwangu ni ndoa ya pili, ya kwanza ilishavunjika na siyo kwamba itakuwa ya mwisho, ila imeshakuwa na mwisho.

Bi harusi naye pambe jamani, akaulizwa kwa nini uhusiano wao umekuwa wa muda mfupi tu na ndoa, yeye akajibu.

"Nampenda sana mume wangu. Sina cha kuongea namshukuru Mungu ndoa ni jambo la heri. Unaweza ukawa na mtu kwa muda mrefu na msiingine kwenye ndoa, lakini mtu sahihi anakuja kwa wakati sahihi."

# Alikiba, Harmonize sasa vita kwenye soka




MSANII nguli nchini wa muziki wa bongo fleva, Ali Kiba anasema angetamani kupambana na Harmonize kwenye mchezo wa mpira wa miguu.

Kiba alisema hayo wakati wa uzinduzi wa Samakiba Foundation, inayofanyika kila mwaka na kuchezwa mechi kati ya timu ya Ali Kiba na staa wa soka nchini na nahodha wa timu ya taifa, Taifa Stars Mbwana Samatta.

Mechi hiyo ambayo hufanyika kila mwaka huwa ni maalum kwa ajili ya mfuko huo ambao baadaye baadhi ya mapato yake huenda kwa wahitaji na wasiojiweza.

"Namualika Harmonize kwenye tamasha hili, na wala simpangii timu, achague mwenyewe timu ya kucheza. Bado sijawasiliana naye moja kwa moja, lakini naanza kwa kusema namualika, niliyewasiliana naye na amethibitisha ni Marioo. Natumia fursa hii kuwakaribisha wasanii wenzangu wanaotaka kujumuika na sisi mlango uko wazi," alisema Kiba.

Ni mechi ya kila mwaka, Kiba akiwa na timu yake akiita Team Kiba, na Samatta upande mwingne akiita Team Samatta, ambapo huchezwa mechi kwa kuwashirikisha wachezaji mbalimbali klabu za Ligi Kuu na maarufu, lakini pia wasanii.

Alisema msimu huu mechi hiyo itachezwa mwezi Julai kwa sababu wachezaji wengi hasa wa Ligi Kuu watakuwa kwenye mapumziko hivyo ni rahisi kupatikana, lakini pia ndiyo wakati wa watalii wengi nchini.

Kiba na Harmonize, mbali na muziki, lakini pia ni wacheza soka wazuri. Kabla ya kuwa msanii, Kiba alizichezea timu mbalimbali jijini Dar es Salaam, lakini baadaye akaamua kujitutuliza kwenye muziki.

Mwaka 2018/19, Kiba aliweka rekodi ya aina yake ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa amesajiliwa na Coastal Union ya Tanga.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICE AKARIBIA UNITED

KLABU ya Manchester United iko tayari kumnunua kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice, mwenye umri wa miaka 24, lakini Arsenal bado inapewa nafasi kubwa ya kumsajili. ***(Guardian)***

### GUENDOUZI KUMRITHI RICE

KIUNGO wa kati wa Marseille na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Matteo Guendouzi, mwenye umri wa miaka 24 anaweza kuchukua nafasi ya Declan Rice katika klabu ya West Ham.(***Mirror***)

### MARTINEZ AGOMBEWA EPL

CHELSEA na Manchester United zimeonyesha nia ya kumsajili mlinda mlango wa Aston Villa na Argentina, Emiliano Martinez, mwenye umri wa miaka 30, huku Tottenham Hotspur pia ikiwa mawindoni kumsaka golikipa huyo. (***Mirror***)

### SILVA KUREJEA FLUMINENSE

CHELSEA itamruhusu mlinzi wa Brazil, Thiago Silva, mwenye umri wa miaka 38, kujiunga tena na Fluminense msimu huu wa joto. (***Telegraph)***

### KIM-JAE KUONDOKA NAPOLI

KLABU ya Manchester United imeanza mazungumzo na beki wa Napoli ambaye ni raia wa Korea Kusini, Kim Min-jae. Liverpool na Paris St-Germain pia zinavutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Foot-Mercato)***

### BELLINGHAM, MADRID SAFI

KIUNGO wa kati wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19 amekubaliana maslahi binafsi na Real Madrid. ***(90min***)

### KULUSEVSKI KUTUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inatarajiwa kukamilisha usajili wa kudumu wa mshambuliaji wa Sweden, Dejan Kulusevski, mwenye umri wa miaka 23 kutoka Juventus msimu huu wa joto. ***(PA via Independent***)

### SPURS KUMNASA IBANEZ

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo tayari kumfanya mlinzi wa AS Roma, Roger Ibanez, mwenye umri wa miaka 24 kuwa usajili wao wa kwanza katika dirisha la msimu wa joto. (***La Repubblica via Four Four Two)***

### DAHOUD HUYO BRIGHTON

BRITGHTON inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili kiungo wa kati wa Ujerumani, Mahmoud Dahoud, mwenye umri wa miaka 27, wakati mkataba wake na Borussia Dortmund utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. (***Fabrizio Romano***)

### LINGARD KUHAMISHA BESIKTAS

KIUNGO wa kati wa Nottingham Forest, Jesse Lingard, mwenye umri wa miaka 30, amepata ofa ya kujiunga Besiktas mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu. (***Nottingham Post***)

### ARSENAL KUMNG'OA SIMAKAN

ARSENAL inavutiwa na mlinzi wa RB Leipzig mwenye umri wa miaka 23, Mohamed Simakan, ambaye alisaini mkataba mpya Desemba, mwaka jana. (***Guardian)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG: WACHEZAJI WAZURI KUTUA UNITED

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amesema "wachezaji wakuu wanataka kuja" Manchester United msimu huu wa joto na amesisitiza dirisha hilo la uhamisho halitegemei klabu hiyo kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**United ipo katika hatari ya kukosa nafasi katika nne bora baada ya kufungwa mfululizo na Brighton na West Ham.**

Lakini Ten Hag anaamini bado anaweza kuvutia wachezaji hapo Old Trafford hata kama hawezi kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**Kocha asema hali imekuwa tofauti na mwaka jana wakati anajiunga na...**

"Naona tofauti kubwa nikilinganisha na mwaka jana," alisema Ten Hag.

"Kulikuwa na kutoridhishwa sana mwaka jana nilipozungumza na wachezaji na sasa wachezaji wengi wanaona mradi, nini kinaendelea, nguvu na matarajio katika mradi huu, ubora haswa.

"Wanatamani sana kuja, nimegundua hilo. Inaonekana kama kulikuwa na kutoridhishwa sana mwaka jana, mashaka mengi tulipokaribia wachezaji. Mwaka huu, wachezaji wengi wenye ubora wanataka kuja."

Ushindi wa mechi tatu katika michezo minne iliyosalia ya United itatosha kuizuia Liverpool na kujihakikishia nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ilikuwa wazi ndivyo ilivyo lakini tunajua ni nini sababu ya hilo," aliongeza.

"Hakika si kisingizio cha uchezaji kama huu lakini pia ni sababu ya kikosi kuonekana kuchoka na kuchoka, niliweza kuona.

"Lakini sasa tumekuwa na wiki, wiki nyingine hadi wiki iliyopita. Nimeona karibu na uwanja wa mazoezi nguvu imerejea. Tutatoa utendakazi bora wa kimwili, nina uhakika na hilo."

SportPesa LIVE IN PLA

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
BRIGHTON
1 | 1.78
X | 3.74
2 | 3.84

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DIABY KUMRITHI MESSI PSG



**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain imeripotiwa ina matumaini ya kuipiku Arsenal katika usajili wa mchezaji, Moussa Diaby, kama mbadala wa Lionel Messi.

Diaby mwenye umri wa miaka 23 anavutia timu nyingi kutokana na kiwango chake katika klabu ya Bayer Leverkusen msimu huu.

Mfaransa huyo amefunga mabao 14 na kutoa asisti 11 msimu huu na kuisaidia timu yake kushika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga.

Diaby alijiunga na kikosi cha Leverkusen akitokea PSG mwaka 2019 kwa ada ya paundi milioni 13.

Na Leverkusen sasa wanaweza kupata faida nzuri, kwa mujibu wa Evening Standard ilisema PSG wanaweza kumrejesha kwa mkataba wa pauni milioni 65.

Miamba hao wa Ligue 1 wanalenga wachezaji chipukizi wa Ufaransa wanapojiandaa kuwaachia Messi na Neymar, ambao wanakabiliwa na mustakabali usio na uhakika hapo Parc des Princes.

# Ramsdale kupewa mkataba mwingine



**LONDON,** England

GOLIKIPA wa Arsenal, Aron Ramsdale, bado yupo sana baada ya taarifa kueleza anakaribia kutia saini mkataba mpya ambao utamweka klabuni hapo kwa muda zaidi.

Ramsdale amekua katika kiwango bora sana kwa misimu miwili aliyoitumikia klabu hiyo haswa ndani ya msimu huu ambapo Arsenal imekua kwenye kiwango bora kabisa.

Lakini vilevile golikipa huyo amekuwa mmoja wa wachezaji ambao ni ufunguo kwenye mafanikio ya timu hiyo msimu huu.

Arsenal ipo kwenye utaratibu wa kuwaongezea mikataba wachezaji wake wanaofanya vizuri klabuni hapo.

Hii imekua sehemu ya mradi wa kuiitengeneza timu hiyo kuwa moja ya timu shindani kwa muda mrefu ndani ya Ligi Kuu England na hata barani Ulaya kwa ujumla.

Taarifa zimeeleza Arsenal imeshamalizana na Ramsdale na inatarajia kumtangaza hivi karibuni kuwa mchezaji huyo ameongeza mkataba wa kuwatumikia washika mitutu hao wa London na kuongeza idadi ya wachezaji walioongeza mkataba klabuni hapo.

CHEZA USHINDE KASINO

# PINTO ACHAGULIWA MJUMBE MPYA MKUTANO MKUU TFF

Na Mwandishi Wetu

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Waandishi wa Habari za Michezo Tanzania (TASWA), Juma Pinto (pichani), amechaguliwa kuwa mjumbe wa mkutano mkuu wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kutoka mkoa wa Dar es Salaam.

Pinto alichaguliwa kwa kupata kura zote za wajumbe wa mkutano mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), katika uchaguzi mdogo uliofanyika kwenye Ukumbi wa hoteli ya Peacock, jana.

DRFA ililazimika kuziba nafasi hiyo kutokana na Shafii Dauda, kufungiwa kutokana na kubainika na makosa ya kimaadili.

"Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote wa mkutano mkuu wa DRFA, ninaahidi nitaenda kuwasilisha mawazo yenu katika mkutano wa TFF na si yangu binafsi," alisema Pinto ambaye alikuwa mgombea pekee wa nafasi hiyo.

Akifungua mkutano huo, Makamu wa Kwanza wa Rais wa TFF, Athumani Nyamlani, aliipongeza DRFA kutoa timu iliyotinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya kimataifa ya Afrika, Yanga ambayo pia ilianza vyema hatua hiyo kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini.

Nyamlani pia aliipongeza DRFA kwa mafanikio yaliyofikiwa na Simba iliyotolea kwenye hatua ya robo fainali na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema mafanikio ya timu hizo mbili katika mashindano ya Afrika ni kilelezo cha kukua kwa soka la Tanzania.

Aliongeza pia utulivu ulioko katika chama hicho kwa sasa ni jambo la kupongezwa na kusema inaakisi mikoa mingine ya Tanzania.

Hata hivyo aliwataka viongozi wa DRFA 'kuamka' na kuendesha mashindano mbalimbali ambayo yatafufua heshima ya mkoa ambao awali ulizalisha wachezaji wengi wanaoshiriki Ligi Kuu.



# *Yanga rasmi bingwa 2022/23*

INATOKA UK. 24

bu Waziri, Hamisi Mwinjuma, pamoja na Watanzania wengine wanaoishi Afrika Kusini.

"Nimeongea na balozi amesema wao pia wamejiiandaa kuwapokea, na wameandaa mabasi kutoka kila mji kuhakikisha Watanzania wanakuwa wengi," alisema Yakubu.

Mtendaji Mkuu wa Yanga, Andrew Ntime, alisema timu yao imejiandaa vizuri kuhakikisha wanapata matokeo chanya na kusonga mbele huku wakiishukuru serikali kwa mchango wake wa kusafirisha mashabiki.

## Simba: Tutasajili vigogo Afrika

INATOKA UK. 24

lekea msimu mpya.

Bosi huyo amesema msimu huu kulikuwa na makosa makubwa ambayo walifanya na kupelekea anguko la timu yaop ambayo lilianza miaka miwili nyuma.

"Wengi wanaangalia anguko letu kwa sasa, lakini anguko letu lilianza miaka miwili nyuma baada ya kuwaruhusu kuondoka Chama (Clatous) na Luis Miquissone hakukuwa na mbadala wao, ukiangalia tumemleta Banda (Peter) ila hakuweza kuziba nafasi yake, tunajipanga kuangalia ni namna gani tutafanya maboresho kwenye kila idara ya timu ili kuwa bora," alisema kiongozi huyo.

Pia amewaomba radhi mashabiki na wanachama wao kwa kukosa mataji katika msimu mwingine huku akitaja majeraha yaliyowapata wachezaji wao muhimu yalichangia kuwaangusha.

"Hakuna wa kumbebesha lawama au kuwaonyesha vidole watu au viongozi waliopewa jukumu la usajili, alitolea mfano Sawadogo (Ismael) alikuwa vizuri katika Ligi ya Morocco, na alikuja Simba alionyesha kiwango kizuri lakini baadaye alipata majeraha na kushindwa kuonyesha ubora wake," bosi huyo alisema.

Aliongeza watafanya usajili mkubwa ambao unaendana na washindani wao huku akiongeza uzoefu wa viongozi na wachezaji utasaidia kutoa ushindani mkubwa katika michuano iliyopo mbele ya Super Cup.

Aliweka wazi Simba imeachana na kocha wa viungo, Kelvin Mandla ambaye ni raia wa Afrika Kusini huku kukiwa na tetesi za kurejeshwa kwa Adel Zrane aliyewahi kufanya kazi hiyo wa mafanikio.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 14/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 1430 | Vitesse Arnhem vs Cambuur | 1.34 | 5.00 | 6.99 |
| 13:30 | 5242 | Verona vs Torino | 2.31 | 3.00 | 3.10 |
| 14:00 | 3049 | Clermont Foot vs Lyon | 3.86 | 3.71 | 1.78 |
| 14:30 | 1186 | Jahn Regensburg vs Hamburger SV | 3.69 | 3.74 | 1.85 |
| 14:30 | 1693 | Paderborn vs Heidenheim | 2.21 | 3.49 | 2.93 |
| 14:30 | 4058 | Hannover vs SV Darmstadt | 3.73 | 3.83 | 1.81 |
| 14:35 | 1695 | Hangzhou NG vs Shanghai SIPG | 4.53 | 3.50 | 1.66 |
| 15:00 | 2847 | Celta Vigo vs Valencia | 2.19 | 3.16 | 3.16 |
| 15:00 | 3549 | Midtjylland vs Horsens | 1.40 | 4.56 | 7.10 |
| 15:00 | 4576 | Gor Mahia vs AFC Leopards | 1.66 | 3.03 | 3.79 |
| 15:15 | 1338 | BSC Young Boys vs FC Zurich | 1.55 | 4.21 | 4.95 |
| 15:30 | 1009 | LASK Linz vs RB Salzburg | 3.28 | 3.49 | 1.93 |
| 15:30 | 2612 | Groningen vs Ajax | 9.97 | 5.98 | 1.22 |
| 15:30 | 4926 | Sturm Graz vs Austria Klagenfurt | 1.25 | 5.14 | 8.43 |
| 16:00 | 1156 | Hammarby vs Djurgardens IF | 2.45 | 3.23 | 2.55 |
| 16:00 | 2662 | Everton vs Manchester City | 6.87 | 4.46 | 1.39 |
| 16:00 | 2959 | Montpellier vs Lorient | 1.80 | 3.65 | 3.85 |
| 16:00 | 3138 | Fiorentina vs Udinese | 1.93 | 3.45 | 3.55 |
| 16:00 | 3295 | Brest vs AJ Auxerre | 2.09 | 3.20 | 3.35 |
| 16:00 | 4302 | Brentford vs West Ham | 2.00 | 3.39 | 3.39 |
| 16:00 | 4643 | Toulouse vs Nantes | 2.08 | 3.50 | 3.10 |
| 16:00 | 4913 | Monza vs Napoli | 4.31 | 3.49 | 1.75 |
| 16:00 | 5507 | Rennes vs Troyes | 1.22 | 6.00 | 9.60 |
| 16:30 | 2710 | Stuttgart vs Bayer Leverkusen | 2.37 | 3.38 | 2.69 |
| 17:00 | 3813 | Brondby vs Copenhagen | 2.94 | 3.40 | 2.27 |
| 17:15 | 3805 | Elche vs Atletico Madrid | 7.57 | 4.78 | 1.34 |
| 17:30 | 4424 | Rio Ave vs Vitoria Guimaraes | 2.50 | 3.10 | 2.75 |
| 17:30 | 5487 | St. Gallen vs FC Basel | 1.84 | 3.73 | 3.67 |
| 17:45 | 3356 | Feyenoord vs GO Ahead Eagles | 1.16 | 6.82 | 12.03 |
| 18:05 | 1486 | Monaco vs Lille | 2.65 | 3.55 | 2.32 |
| 18:30 | 1169 | RB Leipzig vs Werder Bremen | 1.22 | 6.01 | 9.42 |
| 18:30 | 2541 | Arsenal vs Brighton | 1.78 | 3.74 | 3.84 |
| 18:30 | 4007 | Halmstads BK vs Malmo | 5.74 | 4.10 | 1.45 |
| 19:00 | 2921 | Aarhus vs Nordsjalland | 2.28 | 3.30 | 3.00 |
| 19:00 | 3103 | Bologna vs Roma | 3.00 | 3.00 | 2.37 |
| 19:30 | 3096 | Valladolid vs Sevilla FC | 2.21 | 3.35 | 2.95 |
| 19:30 | 3352 | Union Saint Gilloise vs Racing Genk | 1.98 | 3.48 | 3.42 |
| 20:00 | 2215 | Ceramica Cleopatra vs Ghazl EL Mahallah | 1.55 | 3.82 | 5.63 |
| 20:00 | 2375 | Sporting Braga vs Santa Clara | 1.19 | 6.24 | 12.08 |
| 20:00 | 5960 | PAOK vs Olympiakos | 2.24 | 3.18 | 3.18 |
| 20:10 | 3413 | Dinamo Zagreb vs HNK Sibenik | 1.17 | 5.75 | 12.31 |
| 21:00 | 2672 | PSV Eindhoven vs Fortuna Sittard | 1.10 | 8.38 | 16.95 |
| 21:00 | 4390 | AZ Alkmaar vs Emmen | 1.31 | 4.99 | 7.99 |
| 21:45 | 3279 | Juventus vs Cremonese | 1.39 | 4.29 | 7.27 |
| 21:45 | 4467 | Marseille vs Angers | 1.17 | 6.43 | 12.05 |
| 22:00 | 1107 | Vasco da Gama vs Santos | 1.86 | 3.32 | 3.82 |
| 22:00 | 1161 | Corinthians vs Sao Paulo | 2.31 | 3.13 | 2.88 |
| 22:00 | 4521 | Libertad Gran Mamore vs The Strongest | 4.87 | 3.63 | 1.62 |
| 22:00 | 5341 | Espanyol vs Barcelona | 4.49 | 3.67 | 1.68 |
| 22:30 | 2854 | Porto vs Casa Pia Atletico | 1.18 | 6.20 | 13.01 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Mei 14, 2023
Nipashe

UK. 21



## Ten Hag: Wachezaji wazuri kutua United



Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahya (juu), akishangilia pamoja na wachezaji wenzake baada ya kufunga bao katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana. Yanga ilishinda mabao 4-2. **PICHA: MTANDAO**

## Simba: Tutasajili vigogo wa Afrika

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema kipaumbele chake ndani ya timu hiyo kwa sasa ni kuonyesha soka safi na la kuvutia, uongozi wa timu hiyo umeweka wazi utakuja kivingine katika msimu ujao, imefahamika.

Kauli hiyo imetolewa baada ya kikosi chao kuonyesha kandanda safi iliyoonyeshwa kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting, iliyomalizika kwa ushindi wa mabao 3-0.

Robertinho aliliambia Nipashe ni jambo jema ni kucheza soka safi na kupata ushindi mnono kwa sababu inaongeza furaha kwa mashabiki.

Kocha huyo alisema mechi ilikuwa ngumu katika kipindi cha kwanza kutokana na wapinzani wao, Ruvu Shooting kucheza vizuri na kutengeneza nafasi ambazo walishindwa kuzitumia baada ya nyota wa Simba kufanya makosa.

Aliongeza aina yake ya ushangiliaji katika mabao ya juzi alikuwa anajaribu kuwapa furaha mashabiki waliojitokeza pamoja na kupitia kipindi kigumu.

"Nimefurahi ushindi wa leo (juzi) kwa sababu mbili, tumecheza vizuri halafu tumepata mabao mengi, hilo ndio kubwa, kuhusu nilivyokuwa nashangilia nilikuwa nawafurahisha mashabiki ambao walikuwa wakiniambia nicheze," alisema Robertinho.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Salim Abdallah 'Try Again', amekiri hawakuwa na msimu mzuri na tayari wanajipanga upya kuja kivingine kue-

INAENDELEA UK. 23

# Yanga rasmi bingwa 2022/23

## ●●● Kukabidhiwa kombe Mbeya, yamsajili Kinzumbi, Diakite tayari kwa...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAADA ya safari ndefu ya msimu mzima, hatimaye Yanga imetetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuiadhibu Dodoma Jiji mabao 4-2 katika mechi kali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana.

**Yalikuwa ni mabao matatu yaliyofungwa kipindi cha pili na wachezaji waliotokea benchi, Mudathir Yahya, aliyepachika mawili na Farid Mussa, huku moja la kipindi cha kwanza likifungwa na mchezaji wa kimataifa wa Zambia, Kennedy Musonda.**

Ilikuwa hoi hoi nderemo na vifijo mara baada ya mwamuzi, Omary Mdoe, kupuliza kipenga cha kumaliza mechi hiyo, ikiashiria tayari Yanga ina pointi 74 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine 15 zilizobaki katika ligi msimu huu.

Mechi hiyo ilihudhuriwa karibuni na viongozi wote wa Yanga na familia zao, wakiongozwa na Rais, Injinia Hersi Said, ambaye aliungana na wachezaji na viongozi wenzake kushangilia ubingwa huo.

Hata hivyo, haikuwa rahisi kwa mabingwa hao na walilazimika kusubiri hadi dakika mbili kabla mechi kumalizika, ndipo walipoandika bao la tatu na la nne likifungwa dakika za majeruhi, na kabla hapo ngoma ilikuwa sare ya 2-2.

Unakuwa ni ubingwa wa pili mfululizo, ikiwapokonya watani zao na ni ubingwa wa 29 katika vipindi tofauti kwa klabu hiyo tangu kuanza kwa mfumo wa ligi mwaka 1965.

Wakati Yanga ikiwa inaongoza kwa kutwaa ubingwa mara nyingi, Simba inashika nafasi ya pili kwa kutwaa mara 22, Mtibwa Sugar imetwaa mara mbili mwaka 1999 na 2000.

Dodoma Jiji ilifanikiwa kusawazisha bao dakika ya 58 lililotiwa ndani ya kamba na Collins Opare, akiunganisha faulo ya Salmin Hoza na alikuwa ni Seif Karihe aliyewaweka roho juu mashabiki wa Yanga uwanjani hapo kwa kupachika bao la pili dakika ya 66 ya mchezo.

Dakika nne baadaye Mudathir alisawazisha bao hilo baada ya kushirikiana kufanya kazi nzuri na nyota aliyeanzia benchi, Clement Mzize, kupasiana ndani ya boksi kabla ya kuukwamisha mpira wavuni.

Dakika ya 88, Farid alifunga bao la tatu lililopatikana kutokana na kona ya Djuma Shaaban iliyozua patashika nguo kuchanika langoni, kabla mpira kujazwa wavuni.

Ni bao lililoonekana kuwanyong'nyesha Dodoma jiji na haikushangaza ilipofungwa bao la nne kwenye dakika nne za nyongeza likipachikwa tena na Mudathir.

Wakati huo huo katika kuanza maandalizi ya msimu ujao mapema, Yanga inatajwa imekamilisha usajili wa wachezaji watatu wa kimataifa ili kuimarisha kikosi chake, imefahamika.

Tayari kutoka Yanga zinasema tayari mabosi wa klabu hiyo wameshakamilisha usajili wa winga kutoka Real Bamako, Cheickna Diakite, Phillippe Kinzumbi wa TP Mazembe na Bruno Gomes kutoka Singida Big Stars.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameweka wazi atasajili wachezaji wachache sana ambao watakuja kuongeza nguvu kutokana na kikosi kipana alichonacho hakihitaji kufumuliwa sana.

Nabi alisema katika usajili huo, moja ya nafasi ambazo anatarajia kuongeza nyota ni eneo la mawinga wa kushoto na kulia.

Katika hatua nyingine, Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo imegharamia mashabiki 55 watakaoondoka nchini leo kwa usafiri wa basi kuelekea Afrika Kusini kwa ajili ya kushangilia Yanga katika mechi ya pili ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji, Marumo Gallants itakayochezwa Jumatano.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Said Yakubu, alisema msafara huo utaungana na Nai-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >